# Nipashe

Jumamosi Julai 18, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580287

The Guardian digital

www.ippmedia.com

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710




## TAKUKURU yaonya wafanyabiashara

UKURASA 3




UKURASA 11

# Membe rasmi mbio za urais

## ACHUKUA

fomu ACT-Wazalendo akimtaja Maalim Seif...

*Endelea uk. 2*




Waziri wa Mambo ya Nje wa zamani, Bernard Membe, akionyesha mkoba wenye fomu za kugombea nafasi ya urais kupitia Chama cha ACT-Wazalendo baada ya kukabidhiwa na Katibu Mkuu wa chama hicho, Ado Shaibu (hayupo pichani), katika ofisi za makao makuu ya ACT Magomeni, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## Magufuli awatumbua wateule waliojitosa mbio ubunge

UKURASA 2

## YALIYOMO

UKURASA WA 4

**KABUDI AFAFANUA KAULI YA 'KUTOLEWA JALALANI'**

WAZIRI wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, ametoa ufafanuzi kuhusu kauli yake kuwa Rais John Magufuli...

UKURASA WA 4

**JKCI, MOI ZAPANDIKIZA KIFAA CHA MOYO KWA MGONJWA WA AJALI**

KWA mara ya kwanza wataalamu wabobezi wa moyo na wazibuaji wa mishipa ya damu wa Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete (JKCI), wamepandikiza kifaa cha kusaidia moyo kufanya kazi vizuri (pacemaker)...

UKURASA WA 5

**BIBI MATATANI TUHUMA ZA KUMCHOMA MOTO MJUKUU**

JESHI la Polisi mkoani Kilimanjaro linamshikilia Daria Frank (55), mkazi wa Mamba wilayani Moshi kwa tuhuma za kumuunguza...

## MBARONI KUUZA MADINI NJE YA SOKO

UKURASA 4





Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store



**MICHEZO** YANGA DIMBANI KUSAKA HESHIMA UK.24

MAONI, KATUNI UK.6

# JPM awatumbua RC na DC wanaosaka ubunge

**Na Mwandishi Maalum**

SIKU moja baada ya kuteua wakuu wapya wa mikoa ya Dar es Salaam na Manyara, Rais John Magufuli amefanya uteuzi wa viongozi wengine wapya wakiwamo mkuu wa mkoa na mkuu wa wilaya.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa kwa vyombo vya habari jana na Kurugenzi ya Mawasiliano Ofisi ya Rais, Ikulu jana, Rais amemteua Dk. Jumanne Fhika kuwa Mkuu wa Mkoa wa Njombe.

Kabla ya uteuzi huo, Dk. Fhika alikuwa Ofisi ya Rais na anachukua nafasi ya Christopher Ole Sendeka. Juzi, Ole Sendeka alichukua fomu kuomba ridhaa ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) kumteua kuwania ubunge wa Simanjiro katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka huu.

Rais Magufuli pia amemteua Dk. Aloyce Nzuki kuwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Maliasili na Utalii. Kabla ya uteuzi huo, Dk. Nzuki alikuwa Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Maliasili na Utalii na anachukua nafasi ya Profesa Adolf Mkenda.

Taarifa hiyo ya Ikulu pia ilibainisha kuwa, Rais Magufuli amemteua Anthony Sanga kuwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji. Kabla ya uteuzi huo, Sanga alikuwa Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji na anachukua nafasi ya Profesa Kitila Mkumbo, ambaye amejitosa kuwania ubunge wa Ubungo.

Vilevile, Rais Magufuli amemteua Dk. Allan Kijazi kuwa Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Maliasili na Utalii. Dk. Allan Kijazi anachukua nafasi ya Dk. Nzuki aliyeteuliwa kuwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Maliasili na Utalii.

Taarifa ya Ikulu ilibainisha kuwa, licha ya uteuzi huo, Dk. Kijazi ataendelea kuwa Kamishna wa Uhifadhi wa Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA).

Rais Magufuli pia amemteua Nadhifa Kemikimba kuwa Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji. Kabla ya uteuzi huo, Kemikimba alikuwa Mkurugenzi katika Wizara ya Maji na anachukua nafasi ya Sanga aliyeteuliwa kuwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji.

Rais pia amemteua Fadhili Juma kuwa Mkuu wa Wilaya ya Geita mkoani Geita. Kabla ya uteuzi huo, Juma alikuwa Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Lindi na anachukua nafasi ya Josephat Maganga ambaye amehamishwa kituo cha kazi na kuwa Mkuu wa Wilaya ya Dodoma.

Maganga anachukua nafasi ya Patrobas Katambi ambaye jana alirejesha fomu ya kuomba kuteuliwa na CCM kuwania ubunge wa Shinyanga Mjini katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka huu.

Wateule wote wanatakiwa kuwapo Ikulu, Chamwino mkoani Dodoma Julai 20, mwaka huu saa 4:00 asubuhi.



Aliyekuwa Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Tanga, Kassim Mbughuni, akirejesha fomu ya kugombea ubunge Jimbo la Tanga Mjini, kwa usafiri wa baiskeli katika ofisi za wilaya hiyo, jana. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Membe ajitosa rasmi urais

**Na Mary Geofrey**

ALIYEKUWA Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Bernard Membe, amechukua rasmi fomu ya kuomba kuteuliwa na Chama cha ACT-Wazalendo kuwania urais wa Tanzania katika Uchaguzi Mkuu wa Oktoba mwaka huu.

Membe (66), alikabidhiwa fomu hiyo jana jijini Dar es Salaam na Katibu Mkuu wa ACT-Wazalendo, Ado Shaibu, ikiwa ni siku moja tangu ajiunge rasmi na kupokewa na chama hicho.

Wakati wa kuchukua fomu jana, Membe aliyebobea katika masuala ya diplomasia, aliambatana na mkewe, akiwa mwanachama wa kwanza wa ACT-Wazalendo kuchukua fomu ya kuomba kuwania urais wa Tanzania katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka huu.

Muda mfupi baada ya kukabidhiwa fomu hizo, Membe alizungumza na waandishi wa habari na kuahidi kuzijaza kwa umakini wa hali ya juu na kuzirejesha siku za karibuni.

Aliwataka wanachama wengine wa ACT-Wazalendo kujitokeza kuchukua fomu za kuwania nafasi hiyo ya juu ya uongozi nchini kwa kuwa chama hicho kina demokrasia.

"Jana (juzi), nilipokea ombi la wanachama na Mwenyekiti wa ACT-Wazalendo, Maalim Seif Sharif Hamadi, kunitaka nigombee urais. leo (jana) asubuhi nimetekeleza wajibu huo kwa vitendo kwa maandishi na kukabidhi kwenye ofisi kwa maandishi. ACT-Wazalendo inaenda chapu chapu, hatuwezi kuchelewa," alitamba.

Membe alisema amekabidhiwa fomu atakazosoma kwa umakini na atazijaza kwa uangalifu mkubwa ili asitokee wa kusema zimekosewa.

"Sisi siyo kama wale wanaoweza kuzuia wanachama wengine kugombea, hizi fomu si zipo nyingi? Kidumu Chama cha ACT-Wazalendo," alisema Membe huku akicheka bila kukitaja chama alichokilenga.

"Kwa leo (jana) waandishi wa habari ninaomba tuelewane, nimelemewa na mzigo huu (fomu za kuwania urais). Nitazijaza na kama kutakuwa na neno lolote la kusema nitasema. Siku ya karibuni sana nitakapokuja kurejesha hizi fomu, nitamwaga cheche mbili tatu."

Mwanadiplomasia huyo alijiunga na chama hicho baada ya kufukuzwa na Chama Cha Mapinduzi (CCM) Februari 28 mwaka huu kwa tuhuma mbalimbali ikiwamo kukiuka kanuni na miongozo ya chama hicho.

**BARUA YA MSAJILI**

Katika hatua nyingine, Mwenyekiti wa Chama cha ACT-Wazalendo, Maalim Seif Sharif Hamad, amesema Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa nchini haiwezi kufuta usajili wa chama hicho kwa sababu kufanya hivyo ni kinyume cha sheria.

Maalim Seif alitoa kauli hiyo jana alipozungumza na wanachama wa chama hicho Jimbo la Mbagala jijini, ikiwa ni maandalizi ya uchaguzi mkuu wa Oktoba mwaka huu.

"Licha ya kuwapo kwa tishio la kufutwa kwa chama hiki, lakini Msajili hataweza kufanya hivyo kwa sababu Sheria ya Vyama vya Siasa nchini, inamzuia kukifuta chama mwaka mmoja kabla ya uchaguzi," alisema Maalim Seif.

Kiongozi huyo ambaye alichukua fomu ya kuomba kupitishwa kuwa mgombea urais wa Zanzibar kupitia chama chake, alisema anahisi kuwa barua iliyotolewa kwa chama hicho kutoka Ofisi ya Msajili ina lengo la kuwatisha wananchi ili wasijiunge na chama hicho.

Alifafanua kuwa tayari chama hicho kimeshamjibu Msajili na kimekuwa kikifanya hivyo (kujibu barua za Msajili) tangu mwaka 2018, lakini hakuwahi kusema hajaridhika na majibu hayo.

"Kwanza, niwatoe wasiwasi wanachama, hawawezi kufuta chama sheria ya nchi inasema tena kaitunga yeye, kwamba katika kipindi cha mwaka mmoja kabla ya uchaguzi, huwezi kukifuta chama. Kwa hiyo, chama chetu kipo salama," alisisitiza Maalim Seif.

Kauli hiyo ya Maalim Seif imetoka ikiwa ni siku tatu tangu Msajili wa Vyama vya Siasa kukiandikia barua chama hicho akidai ukiukwaji wa Sheria ya Vyama vya Siasa na hatua ambazo atazichukua.

Barua hiyo iliyoandikwa Julai 14 mwaka huu na kutiwa saini na Naibu Msajili wa Vyama vya Siasa, Sisty Nyahoza, iligusia kusudio lake la kutaka kukipa adhabu chama hicho kwa kosa la kukiuka Sheria ya Vyama vya Siasa.

"Msajili wa Vyama vya Siasa anakusudia kuwapa adhabu chini ya Sheria ya Vyama vya Siasa, ili iwe fundisho kwenu na kwa vyama vya siasa vingine kuwa, ni muhimu kuheshimu sheria za nchi ikiwamo Sheria ya Vyama vya Siasa katika shughuli za kisiasa na vyama vya siasa, hasa katika kipindi hiki cha uchaguzi.

"Kutokana na ukweli kwamba, tangu mwaka 2018 ACT-Wazalendo, mmefanya vitendo kadhaa vya kukiuka Sheria ya Vyama vya Siasa na Msajili wa Vyama vya Siasa amekuwa akiwaasa muache kufanya hivyo, lakini hamzingatii ushauri wake," inasomeka sehemu ya barua hiyo.

Miongoni wa makosa yaliyotajwa katika barua hiyo ni kitendo cha kiongozi wa chama hicho, Zitto Kabwe, kuiandikia barua Benki ya Dunia (WB), kuomba isitishe kuipa mikopo Tanzania.

# TAKUKURU yaonya wafanyabiashara kufadhili wanasiasa Uchaguzi Mkuu

**Na Mary Geofrey**

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), imewataka wafanyabiashara kujiepusha na vitendo vya rushwa kwa dhana ya kufadhili gharama za uchaguzi ndani ya vyama vya siasa.

Mkurugenzi Mkuu wa taasisi hiyo, Brigedia Jenerali John Mbungo, alitoa tahadhari hiyo jana jijini Dar es Salaam, alipofungua warsha ya wadau wa uchaguzi, kujadili namna ya kudhibiti vitendo vya rushwa kwenye Uchaguzi Mkuu wa Oktoba mwaka huu.

Brigedia Jenerali Mbungo alisema gharama za uendeshaji wa uchaguzi ndiyo chanzo cha vitendo vya rushwa na baadhi ya wafanyabiashara hutumia mwaya huo kujinufaisha baada ya wagombea waliowafadhili, kupata uongozi serikalini.

"Wapo wagombea wa vyama vya siasa ambao wamekuwa wakichangiwa na watu wenye fedha na hasa wafanyabiashara, ili kudhamini mchakato na baada ya uchaguzi watu hao wachache wenye uwezo hujipatia manufaa zaidi pindi wagombea hao wanapoingia kwenye madaraka," alisema. Brigedia Jenerali Mbungo alisema vitendo hivyo vinasababisha viongozi kufanya uamuzi wa kisera wenye maslahi kwa watu wachache.

"Mara nyingi chanzo kikuu cha rushwa katika uchaguzi ni gharama za uchaguzi. Jambo hili husababisha wagombea au watia nia kutumia ushawishi pamoja na nguvu ya fedha ili kurubuni wapigakura wawachague.

"Mgombea au wagombea wenye uwezo wa kifedha, hutumia kigezo hicho cha fedha kuwarubuni wananchi ili wawachague," alisema Brigedia Jenerali Mbungo. Alisema TAKUKURU iliamua kukutana na wadau wa uchaguzi kwa lengo la kuunga mkono azma ya Rais John Magufuli ya kutaka uchaguzi huo ufafanyike kwa haki, huru na usawa.

Alisema Juni 26 mwaka huu wakati Rais Magufuli anavunja shughuli za Bunge la 11, alisisitiza wadau wa uchaguzi kuepuka vitendo vya rushwa katika uchaguzi huo.

"Kwa kuzingatia katiba ya nchi inayoelekeza taasisi na vyombo vyote, tunaelekeza nguvu na juhudi kuhakikisha tunaondoa rushwa katika jamii yetu. TAKUKURU imeelekeza nguvu katika hili," alisema.

Kiongozi huyo wa TAKUKURU alisema rushwa ina athari kubwa katika mchakato wa uchaguzi na kwa kulitambua hilo, taasisi hiyo ni lazima iidhibiti.

Alisema athari hizo ni wananchi kukosa viongozi wawajibikaji, waadilifu na wazalendo, uvunjifu wa amani kutokana na migogoro ya mara kwa mara ya kisiasa na taifa kugubikwa na rushwa.

Brigedia Jenerali Mbungo alisema rushwa pia inadidimiza uchumi wa taifa kutokana na ukosefu wa mipango ya maendeleo, kukosekana kwa uwazi katika kufanya uamuzi, utawala bora pamoja na wananchi kukosa imani na serikali yao.



Wakili Erick Kidyalla (kulia), akirejesha fomu za kuomba ridhaa ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya kugombea ubunge wa Jimbo la Kibamba kwa katibu wa chama hicho, Wilaya ya Ubungo, Sylevester Yared, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# 'Wanaogombea wajiuzulu utumishi'

**Na Enock Charles**

MTANDAO wa Watetezi wa Haki za Binadamu, amewataka watu wote wanaogombea nafasi mbalimbali za uongozi huku wakiwa na nafasi katika utumishi wa umma, kujiuzulu nafasi hizo, ili kutosababisha mgongano wa kimaslahi.

Umesema suala hilo limewekwa bayana kwenye Sera ya Utumishi wa Umma inayowataka watia nia kuachia nafasi zao ili kutoleta mgongano wa kimaslahi katika nafasi wanazogombea na taasisi wanazoziongoza.

Mratibu wa Mtandao huo, Onesmo Ole Ngurumwa, alisema jana kuwa ni vizuri kutenganisha taasisi na maslahi binafsi, ili kujenga kuaminika kwa taasisi hizo kwa wananchi. "Upokwenda kugombea kama una nafasi fulani ya umma, ni vyema ukajiuzulu ili watu waelewe kuwa alikwenda kugombea ni wewe peke yako wala siyo taasisi unayofanya kazi.

"Bila kufanya hivyo, inaleta picha kwamba amekwenda kugombea nafasi fulani huku akiwa anapata sapoti ya taasisi yake au kwa namna moja au nyingine anatumia rasilimali za taasisi yake," Ole Ngurumwa alisema.

Mratibu huyo alimpongeza Rais John Magufuli kwa kuwaondoa katika nafasi za uongozi viongozi mbalimbali wa umma waliojitokeza kuwania nafasi za kisiasa ikiwamo ubunge, akisema ameonyesha mfano bora ambao ulikuwa haufanyiki katika uchaguzi uliopita.

Alisema katika taasisi hiyo, wameweka utaratibu wa watu kujiuzulu wapojitokeza kuwania nafasi za kisiasa ili kuhakikisha kwamba panakuwa na uwajibikaji katika taasisi hiyo na kuziomba taasisi nyingine kuiga mfano huo, ili kuzuia wafanyakazi kuchanganya siasa na kazi zao za umma kwa kuwa na mawazo ya kisiasa kila wakati.

Katika waliojitokeza kuwania ubunge na udiwani katika uchaguzi mkuu wa mwaka huu wamo pia viongozi wa taasisi mbalimbali za umma na watumishi katika idara mbalimbali za taasisi hizo ambao baadhi yao wamekwisha tangaza kujiuzulu nafasi zao.

## DC anayewania ubunge atumbuliwa, ashukuru

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

ALIYEKUWA Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Patrobas Katambi, ameeleza sababu ya kuchukua fomu kuomba ridhaa ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) kuteuliwa kuwania ubunge wa Shinyanga Mjini.

Katambi amesema iwapo atafanikiwa kuteuliwa na chama na kushinda ubunge katika jimbo hilo, ataisaidia Shinyanga kupata maendeleo kama alivyofanya Dodoma.

Jana, Rais Magufuli alimteua Joseph Maganga kuwa Mkuu wa Wilaya Dodoma, kuchukua nafasi ya Katambi. Baada ya Ikulu kutoa taarifa ya uteuzi huo, Katambi alimshukuru Rais Magufuli kwa kumwamini na kumteua kuwa mkuu wa wilaya, akitumikia nafasi hiyo kwa miaka miwili.

Alisema tangu alipoingia jijini Dodoma mwaka 2018, amefanya kazi kubwa za kimaendeleo na kuubadilisha mji huo, na anaona sasa ni zamu ya wanaShinyanga kuwaletea maendeleo.

Katambi alisema shauku ya kuipatia maendeleo Shinyanga ndiyo imemsukuma kuchukua fomu ya kuomba ridhaa ya kuteuliwa kugombea ubunge katika Jimbo la Shinyanga Mjini.

"Nimerudisha fomu ya kuomba ridhaa ya kuteuliwa na CCM kugombea ubunge katika Jimbo la Shinyanga Mjini. Nimepata mrithi wangu kwenye kituo cha kazi Dodoma, na ninamshukuru sana Rais John Magufuli, aliniamini na kunipatia ukuu wa wilaya.

"Nimedhamiria kuja kuleta maendeleo hapa mjini Shinyanga kama nilivyofanya Dodoma, yaani nimejitoa sadaka kuuacha ukuu wa wilaya kwa ajili ya maslahi ya wanaShinyanga, hivyo waniamini na kunipatia ubunge, ili niwatumikie," alisema.

Katambi alisema kuwa, endapo akikosa ubunge japo hategemei kuukosa, atakwenda kufanya shughuli zingine zikiwamo zinazohusu taaluma yake ya sheria.

Hadi jana mchana, kuliwa na makada 53 wa CCM waliokuwa wamejitosa kuwania ubunge wa Shinyanga Mjini, akiwamo aliyekuwa Mbunge wa Jimbo hilo, Stephen Masele.

# JKCI, MOI zapandikiza kifaa cha moyo kwa mgonjwa wa ajali

**Na Joseph Mwendapole**

KWA mara ya kwanza wataalamu wabobezi wa moyo na wazibuaji wa mishipa ya damu wa Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete (JKCI), wamepandikiza kifaa cha kusaidia moyo kufanya kazi vizuri (pacemaker) nje ya taasisi hiyo bila ya kutumia mtambo wa Cathlab.

Mgonjwa aliyewekewa 'pacemaker' alipata ajali iliyosababisha uti wa mgongo kupata shida na kusababisha baadhi ya viungo vya mwili kupoteza uwezo wa kufanya kazi ikiwamo mishipa ya damu inayoratibu uwezo wa moyo kutengeneza mapigo yake.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, daktari bingwa wa magonjwa ya moyo wa JKCI, Yona Gandye, alisema kutokana na tatizo alilolipata mgonjwa baada ya kupata ajali, mapigo ya moyo yalishuka hadi kufikia 30 kwa dakika na kuonyesha dalili za ukosefu wa mahitaji muhimu ya mwili yanayosambazwa na mapigo ya moyo ambayo ni oksijeni, virutubisho, madini na chakula.

"Mgonjwa huyo alikuwa amelazwa katika Taasisi ya Mifupa Muhimbili (MOI) na alihitaji huduma ya haraka ya kuwekewa kifaa kisaidizi ambacho kinausaidia moyo kufanya kazi vizuri ili mapigo yafikie 60 hadi 100 ambayo ni mapigo ya kawaida ya moyo".

"Kutokana na mazingira ya mgonjwa kutohamishika kutoka MOI na kuletwa JKCI, ilibidi tumfuate kumwekea 'pacemaker'. Tulitumia vyumba vya upasuaji vya kawaida kutumia mashine tofauti na yetu ambayo yao inajulikana kwa jina la C-ARM," alisema.

Dk. Gandye alisema huduma hiyo wameitoa kwa mara ya kwanza nje ya taasisi hiyo na kuifanya bila ya kutumia mtambo wa Cathlab (Catheterization Laboratory) ambao ni maabara ya uchunguzi wa mishipa ya damu ya moyo na tiba.

# Kabudi afafanua kauli ya kutolewa 'jalalani'

**Na Enock Charles**

WAZIRI wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, ametoa ufafanuzi kuhusu kauli yake kuwa Rais John Magufuli amemtoa jalalani.

Profesa Palamagamba Kabudi amesema kauli hiyo haikulenga kukidhalilisha Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) alikokuwa anafanya kazi kabla ya kuteuliwa na Rais John Magufuli kuwa waziri, bali ililenga kutoa shukrani kwa kiongozi huyo wa nchi kwa kumkumbuka katika uteuzi wake.

Katika mahojiano na Kituo cha Televisheni cha Wasafi juzi, Profesa Kabudi ambaye ni miongoni mwa wabobezi katika taaluma ya sheria nchini, alitolea ufafanuzi kauli yake hiyo, akisema kamwe UDSM haiwezi kuwa jalala.

Mwaka mmoja uliopita, Profesa Kabudi alitoa kauli hiyo ambayo tafsiri zake ziliibua ukakasi, baadhi wakiihusisha na udhalilishaji dhidi ya UDSM, chuo kikuu kikongwe zaidi nchini.

Hata hivyo, katika ufafanuzi wake, Profesa Kabudi anasema hakukusudia kukidhalilisha chuo kikuu hicho kwa kuwa hakiwezi kuwa jalala kama ilivyotafsiriwa.

Waziri huyo alisema nafasi aliyopewa na Rais Magufuli hakuitarajia licha ya kuwa msomi mzuri aliyesoma ndani na nje ya nchi na kufikia hatua ya kufundisha UDSM.

"Wapo waliosema mtoto wa mwalimu, baba na mama walimu, hawezi kutoka jalalani," Profesa Kabudi alisema na kufafanua zaidi kwamba:

"Na niseme Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ni moja wa wanufaika wa mazungumzo yetu na Barrick. Kwa muda wa miaka 10, Kampuni ya Barrick itakipa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam Dola milioni 10. Sasa, ingekuwa ni jalala, ningetafuta fursa hiyo? Profesa Kabudi alihoji.

Tayari mtaalamu huyo wa sheria amechukua fomu ya kuwania ubunge katika Jimbo la Kilosa mkoani Morogoro, akiahidi kupeleka maendeleo kwa wananchi wa jimbo hilo kwa kuwa mkoa huo ni wa kimkakati.

Profesa Kabudi ni miongoni mwa waliokuwa wabunge wa kuteuliwa na Rais katika Bunge la 11, waliotia nia ya kuwania ubunge katika Uchaguzi Mkuu wa Oktoba mwaka huu.

Wengine ni Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango, aliyejitosa kusaka nafasi ya kuteuliwa kuwania ubunge wa Buhigwe mkoani Kigoma na Naibu Spika, Dk. Tulia Ackson, aliyechukua fomu kuomba ridhaa ya CCM kugombea ubunge Jimbo la Mbeya Mjini.




Wanafunzi wa Shule ya Msingi Mahaha katika Halmashauri ya Mji wa Bariadi, mkoani Simiyu, wakiwa wamebeba ndoo za maji ambazo hutokanazo nyumbani kila siku kwa ajili ya kubeba maji ya kunawa mikono ili kujikinga na maambukizi ya ugonjwa wa corona, shuleni hapo jana. **PICHA: HAPPY SEVERINE**

# Mbaroni madai kuuza dhahabu kwa magendo

**Na Mohab Dominick,** SHINYANGA

WATU saba wanashikiliwa na Jeshi la Polisi mkoani Shinyanga kwa tuhuma za kuuza dhahabu nje ya masoko yaliyoanzishwa kwa mujibu wa sheria na serikali kwa lengo la kuwawezesha wachimbaji wadogo kunufaika na uchimbaji huo.

Kaimu Kamanda wa Polisi Mkoa wa Shinyanga, Kamishna Msaidizi (ACP) Joseph Paul, alisema jana kuwa tukio hilo lilitokea Julai 14, mwaka huu, majira ya saa 1:00 usiku katika machimbo ya Mwakitolyo wilayani Shinyanga.

Alisema Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na Tume ya Madini Mkoa wa Shinyanga, liliwakamata watu watano wakiwa na gramu 11.4 za dhahabu wakiwa wanafanya biashara nje ya soko la madini jambo ambalo ni kukiuka sheria za madini na kuifanya serikali ipoteze mapato.

Kwa mujibu wa Paul, watu hao watafikishwa mahakamani kwa hatua zaidi ili sheria ichukue mkondo wake huku akitumia nafasi hiyo kuwaonya wafanyabiashara wa madini kutoendelea na mchezo huo kwa kuwa serikali haitawafumbia macho.

Aliwataka wafanyabiashara kufuata utaratibu uliowekwa na serikali ili wao wenyewe wanufaike na raslimali hizo badala ya kukwepa au kutorosha madini hayo kwa sababu masoko yamefunguliwa kila mahali kwa hiyo wafanye hivyo ili kupata bei nzuri, lakini serikali nayo ipate mapato.

Ofisa Madini Mkoa wa Shinyanga, Mhandisi Joseph Kumburu, akizungumza na waandishi wa habari waliofika ofisini kwake, alisema kutokana na tukio hilo, Ofisi ya Madini Mkoa wa Shinyanga, ilipata taarifa kutoka kwa raia wema kuwa kuna baadhi ya watu wanaendelea kufanya biashara ya dhahabu nje ya utaratibu wa masoko.

Mhandisi Kumburu alisema watu hao wametenda kosa kwa kukiuka kifungu cha 6 cha Kanuni za Masoko za mwaka 2019.

Alisema baada ya kupata taarifa hizo, Tume ya Madini ilishirikiana na vyombo vya ulinzi na usalama na kuweka mtego katika operesheni hiyo iliyofanyika eneo la Mwakitolyo.

"Katika operesheni hiyo, tuliwakamata watuhumiwa saba katika eneo la Mwakitolyo namba 1, 2 na 3. Watuhumiwa hao walikutwa wakinunua dhahabu nje ya soko huku mmoja akikamatwa akiwa na gramu sita na mtuhumiwa mwingine gramu 2.6," alisema.

Kumburu aliwataja watuhumiwa hao kuwa ni Matingwa Matembe (56), Magida Magida (38), Makomba Maduhu (40), Malugu Nzemi (45), Kija Ndakile (44), Daud Soni (32) na Singu Legele (37).

Alisema tukio hilo ni la pili na kwamba operesheni kama hiyo ilifanyika na kukamatwa kwa vijana sita ambao baadaye walikiri makosa yao na kulipa kodi zote za serikali na adhabu kwa hiari yao.

Kwa mujibu wa ofisa huyo, operesheni hizo zimesaidia kuongezeka upatikanaji wa dhahabu kwenye kituo kutoka gramu 300 hadi wastani wa gramu 1,000 kwa siku sambamba na kuongezeka kwa madalali kwenye kituo cha soko.

Pia alisema operesheni hizo zimesaidia kupungua kwa utoroshaji wa madini baada ya kupungua kwa wanunuzi wasio rasmi.

# Bibi matatani tuhuma za kumchoma moto mjukuu

**Na Mary Mosha, MOSHI**

JESHI la Polisi mkoani Kilimanjaro linamshikilia Daria Frank (55), mkazi wa Mamba wilayani Moshi kwa tuhuma za kumuunguza na moto mtoto wa miaka sita kuanzia chini ya kitovu hadi juu ya magoti.

Kamanda wa Polisi mkoani Kilimanjaro, Emmanuel Lukula, alisema jana kuwa tukio hilo lilitokea Julai 10, mwaka huu, majira ya saa 11:00 jioni katika maeneo ya Mamba.


Lukula alisema mtuhumiwa huyo ambaye ni bibi mzaa baba wa mtoto huyo, alimfanyia kitendo hicho cha ukatili mtoto huyo (jina linahifadhiwa) ambaye ni mwanafunzi wa chekechea katika Shule ya St. Paul Albert.

Alisema wakati akiendelea kuungua na moto, majirani walisikia kelele za vilio kutoka kwa mtoto huyo na kujitokeza kwa ajili ya kutoa msaada na kufanikiwa kuuzima kwenye mwili wa mtoto.

Kamanda Lukula alisema moto huo tayari ulishamjeruhi vibaya mtoto huyo mwilini mwake na kwa sasa amelazwa katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa ya Mawenzi kwa matibabu zaidi akitokea Hospitali ya Marangu alikopatiwa matibabu ya awali huku mtuhumiwa akishikiliwa na Jeshi la Polisi.

Katika tukio lingine lililotokea Julai 16, mwaka huu majira ya saa 10:00 jioni, polisi wakiwa katika doria walimkamata Mosses Swai (44) mkazi wa Usa jijini Arusha akiwa na dawa za kulevya aina ya bangi mifuko 15 zenye uzito wa kilogramu 379.

Lukula alisema mtuhumiwa alikamatwa maeneo ya njia panda ya Kilema wilayani Moshi akisafirisha kwa kutumia gari lenye namba za usajili T 802 AFZ aina ya Toyota Hiace, linalofanya safari kutoka Moshi Mjini kwenda Holili na kwamba bangi hiyo ilikuwa ikisafirishwa kutoka Moshi kwenda Kenya.




Mkuu wa Wilaya ya Chunya mkoani Mbeya, Samwel Jeremiah (wa pili kushoto), akikabidhi msaada wa mabati 350 kwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Songwe, mkoani Songwe, Faudhia Hamidu yalitolewa na Benki ya NMB, Kanda ya Nyanda za Juu, kwa ajili ya ujenzi wa Sekondari ya Kaloleni na zahanati ya Manda mkoani Songwe, juzi. Wa (pili kulia) ni Meneja wa Benki ya NMB, Kanda ya Nyanda za Juu, Straton Chilongola. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## JPM amtumbua Kafulila

**Na Mary Geofrey**

RAIS John Magufuli, amefanya uteuzi wa viongozi mbalimbali akiwamo Dk. Seif Shekilage, anayekuwa Katibu Tawala wa Mkoa wa Songwe, akichukua nafasi ya David Kafulila.

Taarifa iliyotolewa jana na Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu, Gerson Msigwa, ilibainisha kuwa, kabla ya uteuzi huo, Dk. Shekilage alikuwa Mkuu wa Wilaya ya Maswa mkoani Simiyu.

Rais Magufuli pia amemteua Mussa Chogelo kuwa Mkuu wa Wilaya ya Ilala mkoani Dar es Salaam, akichukua nafasi ya Sophia Mjema, huku akimteua pia Aswege Kaminyonge kuwa Mkuu wa Wilaya ya Maswa mkoani Simiyu.

Kabla ya uteuzi huo, Kaminyonge alikuwa Ofisa Utumishi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali mkoani Mbeya, anayechukua nafasi ya Dk. Shekilage ambaye ameteuliwa kuwa Katibu Tawala wa Mkoa wa Songwe.

Vilevile, Rais Magufuli amemteua Calorious Misungwi kuwa Mkuu wa Wilaya ya Kalambo mkoani Rukwa na kabla ya uteuzi huo Misungwi alikuwa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) na anachukua nafasi ya Bunyura.

Rais Magufuli pia alimteua Dk. Athuman Kihamia kuwa Mkuu wa Wilaya ya Rombo mkoani Kilimanjaro. Kabla ya uteuzi huo, Dk. Kihamia alikuwa Ofisi ya Rais na anachukua nafasi ya Agness Hokororo, huku akimteua Lainie Kamendu kuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kilolo mkoani Iringa kuchukua nafasi ya Aloyce Kessy.

Katika hatua nyingine, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Gorge Mkuchika, amemteua Hanan Bafagil kuwa Katibu Tawala wa Wilaya ya Arusha.

Kabla ya uteuzi huo, Bafagil alikuwa Ofisa Tarafa wa Kinondoni jijini Dar es Salaam na anachukua nafasi ya David Mwakiposa Kihenzile. Wateule wote wataapishwa Ikulu, Chamwino mkoani Dodoma Jumatatu kuanzia saa 4:00 asubuhi.

# Wapewa mafunzo ya kukabili vifo vya uzazi

**Na Neema Emmanuel,** MWANZA

MADAKTARI, wauguzi na wakunga 35 wapewa mafunzo ya namna ya kutoa huduma bora kwa wajawazito na watoto na kuondokana na hofu ya kupata maambukizi ya virusi vya corona pindi wanapotoa huduma, ili kuepusha vifo vitokanavyo na uzazi.

Meneja Mradi wa Impact Mkoa wa Mwanza, Edna Selestine, alisema wamelazimika kutoa elimu hiyo ili kuwafikia watoa huduma ngazi zote, ikiwa ni sehemu ya mikakati yao ya kushirikiana na serikali kupunguza vifo vya uzazi na watoto wachanga nchini.

Alisema mradi huo uko chini ya Taasisi ya Maendeleo ya Aga Khan (AKDN) na umefadhiliwa na Serikali ya Canada (Global Affairs Canada), ukifanya kazi katika halmashauri nane za mkoani Mwanza.

Alisema kuwa, kupitia mradi huo, kumejengwa majengo 28 kwa ajili ya huduma ya mama na mtoto, yakiwa na vyumba vya upasuaji na elimu hiyo wanayoitoa kwa wawezeshaji hao ambao watatembelea vituo mbalimbali vya afya kutoa elimu, itasaidia kupunguza vifo.

"Leo tumewapa na vifaa tiba venye thamani ya Sh. milioni 4.3 ambavyo watavitumia kujikinga wao pindi wanapoenda kutoa huduma. Vilevile, vifaa hivyo watavitumia kuelimishia wengine namna watakavyovitumia pindi wanapoenda kutoa huduma," alisema.

Dk. Colomba Mbekenga, Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Aga Khan, Shule ya Uuguzi na Ukunga, alisema kuwa mkoani Mwanza, mradi wao unahudumia vituo 80, hivyo wauguzi hao wanaopewa mafunzo, watagawiwa vituo vya kazi ambavyo watakuwa wanavizungukia kila mwezi kutoa elimu waliyoipata ili kuitoa kwa watoa huduma wengine.

Claudia Kaluli, Muuguzi Mkuu wa Mkoa, akizungumza kwa niaba ya Mganga Mkuu wa Mkoa, alisema Impact wamewasaidia kwa mambo mengi ikiwamo kutoa elimu kwa watumishi wao na kuwasomesha baadhi ya watumishi kwa mwaka mzima kozi ya kutoa dawa ya usingizi.

Alisema kitengo cha usingizi kilikuwa na upungufu mkubwa kwa wataalamu na kwamba Impact wajenga majengo ya wazazi na huduma za uzazi baada ya kujifungua katika vituo mbalimbali. Dk. Raymond Nyasebwa, daktari mwezeshaji kutoka Hospitali ya Wilaya ya Misungwi na Salome Ngeleja, Ofisa Muuguzi Hospitali ya Mkoa ya Sekou-Toure, walisema elimu waliyoipata imewajenga upya, kuwaongezea ufahamu na kuwaondolea hofu ya corona.

"Wito wetu kwa jamii ni kuendelea kujikinga na kuzingatia maelekezo ya Wizara ya Afya kila wakati na kuondokana, lazima tuendelee kujikinga," alisema Ngeleja.

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Maandalizi sahihi yatazaa msimu imara wa 2020/21

**MSIMU** wa 2019/20 hapa nchini unatarajiwa kumalizika rasmi ifikapo Agosti 2, mwaka huu kwenye Uwanja wa Nelson Mandela, ulioko Sumbawanga Mjini, mkoani Rukwa.

Pazia hilo la msimu litafungwa kwa mechi ya fainali ya Kombe la FA, kati ya Simba ya jijini, Dar es Salaam dhidi ya Namungo FC kutoka mkoani Lindi.

Kwa sasa timu zinazoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara zimebakisha mechi tatu ili kumaliza msimu wakati Ligi Daraja la Kwanza inatarajiwa kukamilika mwishoni mwa wiki hii kwa mechi za mtoano.

Bingwa wa Ligi Daraja la Kwanza atapatikana leo baada ya kumalizika kwa mchezo wa fainali kati ya Gwambina FC ya jijini Mwanza dhidi ya klabu kutoka makao makuu ya Tanzania, Dodoma Jiji FC.

Kumalizika kwa msimu huo, ni dalili kwamba maandalizi ya msimu mpya yanatakiwa kuanza mapema na maandalizi bora au sahihi huanzia kwa timu kufanya usajili imara kwa kufuata mapendekezo yaliyotolewa na benchi la ufundi.

Mafunzo kwa waamuzi na semina elekezi kwa viongozi, pia ni sehemu mojawapo inayotakiwa kufanyiwa kazi kuelekea msimu mpya wa mwaka 2020/21.

Hata hivyo, jambo kubwa ambalo hubeba matokeo yote ni suala la kanuni ambazo hutarajiwa kutumika katika kufanya maamuzi mbalimbali.

Nipashe inawakumbusha viongozi wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), pamoja na wadau wengine wanaoshiriki katika kuandaa kanuni kuhakikisha mnazitendea haki kanuni hizo kwa kuangalia mazingira halisi.

Kanuni zinazotakiwa kupitishwa ni zile ambazo zitasaidia wengi na si ambazo zitawafurahisha wadau wachache.

Kwa kupitisha kanuni bora, kutasaidia msimu ujao wa Ligi Kuu Bara, Ligi Daraja la Kwanza, Ligi Daraja la Pili na mashindano ya Kombe la FA kufanyika kwa kiwango bora.

Muhimu ni viongozi kupitisha kanuni mpya kwa kuangalia mapungufu yaliyojitokeza katika msimu uliopita.

Ukiondoa kanuni, suala la upangaji wa ratiba za ligi umekuwa ni donda sugu hapa nchini kwa baadhi ya timu kupangiwa ratiba inayoumiza huku klabu nyingine zikinufaika na ratiba hizo zinazotolewa na Bodi ya Ligi ambayo iko chini ya TFF.

Tunaamini suala la baadhi ya timu kuwa na mechi za viporo, msimu ujao halitaonekana au halitakuwa gumzo huku mapumziko baina ya mechi moja na nyingine yakiwa sawa kwa klabu zote.


Maandalizi haya yakienda vema, Nipashe inaamini mwisho wa msimu bingwa atakayepatikana atakuwa ni wa halali na atakapokwenda kupeperusha bendera ya nchi kwenye mashindano ya kimataifa atachuana vema na hatakuwa msindikizaji.

Mbali na wachezaji kushindwa kucheza kwa kiwango cha juu, mechi za viporo zinaonekana kutengeneza mazingira ya kupanga matokeo, lakini vinapunguza ushindani baina ya timu kwa sababu tayari safari ya ubingwa huonekana kwa timu zinazopambana kuwania taji hilo.

Kujifunza au kugeza kwa nchi zilizoendelea si dhambi, huu ni wakati mwingine kwa TFF na maofisa wake wote wanaoandaa kanuni kujipanga kupitisha kanuni zitakazosaidia maendeleo ya soka hapa nchini.

Ni ukweli kikosi cha Timu ya Taifa (Taifa Stars) ambacho mwakani kitashiriki fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN), kinategemea wachezaji wanaotoka kwenye ligi hiyo na si mahali kwingine.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

# Morrison ni nani Yanga?



Na Barnabas Maro

**"HESHIMA** apewe ajuwaye heshima." Ni vizuri kumheshimu mtu anayewaheshimu wenzake. Hii ni methali ya kutumiwa kutushauri kuwa tunapaswa kuwaheshimu wale wanaoweza kutuheshimu. 'Adabu' ni utaratibu unaokubalika katika kufanya jambo; heshima, nidhamu.

Kwa hiyo heshima haiji mpaka iletwe. Maana yake heshima haiwezi kuwapo bila ya kuletwa. Methali hii pia yaweza kutumiwa kwa kumsuta mtu anayetaka apewe heshima ingawa vitendo vyake havielekei au mwenyewe haelekei kujiheshimu.

Vilevile heshima ni kitu cha bure. Maana yake heshima hainunuliwi. Hii nayo ni methali ya kutumiwa kutunasihi tuwe na heshima na adabu.

Timu ya mpira wa miguu huwa na wachezaji 11 uwanjani wanaotakiwa kucheza kwa bidii na ushirikiano ili kupata ushindi dhidi ya timu pinzani. Haijatokea wala haitatokea mchezaji mmoja tu kuingia uwanjani ili ashindane na timu yenye wachezaji 11.

Itakuwa mshangao, kioja na kichekesho kwa watazamaji na waamuzi kuona mchezaji mmoja tu anaingia uwanjani kupambana na timu pinzani yenye wachezaji 11! Mchezo huo hautachezeshwa na timu ya mchezaji husika itawajibika mbele ya sheria za mashindano.

Pele, aliyekuwa mchezaji mahiri wa kabumbu nchini Brazil, alisifika duniani kote kwa umahiri aliokuwa nao uwanjani mpaka akaitwa 'mfalme' wa kabumbu duniani, lakini alihitaji msaada na ushirikiano na wachezaji wenzake. Ndio maana wahenga walisema "Kidole kimoja hakivunji chawa."

Maana yake mtu hawezi kumvunja chawa kwa kidole kimoja, lazima akihusishe na kingine.

Bernard Morrison ni mchezaji wa Yanga mwenye asili ya Ghana. Hajui maana ya ushirikiano, heshima na adabu? Au anadhani yeye ndiye mchezaji bora zaidi ya wengine woote aliowakuta Yanga? Hajui kuwa Yanga ilianzishwa mwaka 1935 wakati yeye hakujulikana kama angezaliwa?

Yanga ilikuwa na wachezaji mahiri na shupavu kuliko yeye lakini hakuna aliyejiona bora kuliko wenzake.

Kama Morrison aliwadharau wachezaji wenzake wa timu zote alizochezea kwao na nchi zingine, si hapa Tanzania. Kutokuwa na adabu kwa viongozi ni huko huko lakini si Tanzania, abadan.

Asidhani kuwa yeye ni bora zaidi ya wachezaji wenzake, walimu na viongozi wa klabu iliyomsajili.

Mchezaji anapotolewa ili aingie mwingine, maana yake ameumia au kashindwa kuendana na kasi ya mchezo. Anapotoka uwanjani hukaa kwenye benchi la wachezaji wa akiba ila anapofanya kosa kubwa na kuoneshwa kadi nyekundu hutakiwa kwenda kwenye chumba cha wachezaji.

Morrison anatolewa uwanjani baada ya kushindwa kuendana na kasi ya mchezo, lakini anakataa kukaa kwenye benchi la wachezaji wenziye wa akiba na kwenda kwenye chumba cha wachezaji, kubadili nguo na kuondoka kabisa uwanjani huku mchezo ukiendelea!

Kuna wakati aliondoka kambini kwa kiburi na alipofuatwa alitishia kwa kisu kisha akaelekea alikokusudia. Kwa kitendo hicho alimdharau kocha, wachezaji wenzake, benchi la ufundi, viongozi wa klabu na watazamaji waliotoa fedha zao kuuangalia mchezo huo.

Nadhani viongozi wa Yanga wanaogopa kumrudi (kitendo cha kumwadhibu mtu kwa kosa alilofanya) Morrison. Kama sivyo, mbona wamekuwa kimya kwa utovu wa nidhamu anaofanya mara kwa mara? Hawajui ukimya wao unazidi kumfanya ajione yeye ni bora zaidi ya wachezaji wenzake na viongozi ambao ndio waliomsajili?

Yanga imecheza mechi nyingi na kushinda bila uwepo wake na imeshindwa akiwa mchezoni. Kwa nini anadekezwa kiasi hicho? Ameikuta Yanga na ataondoka aiache ikiitwa Yanga, sio Morrison! Utovu wa nidhamu anaofanya Yanga uwe fundisho kwa timu zinazotaka kumsajili.

Nionavyo, viongozi wa Yanga wamekuwa kimya sana kiasi cha kudharauliwa si na wanachama tu bali hata mashabiki! Tangu uongozi wa sasa uingie madarakani umekuwa kimya sana. Matokeo yake wadhamini wa Yanga, GSM sasa ndio kila kitu. Wanasajili na ndio wasemaji na watendaji!

Uongozi ni dhamana ya kusimamia jambo kwenye taasisi au penginepo; madaraka anayopewa mtu kusimamia au kuongoza shughuli. Viongozi wa Yanga hawasikiki. Wanamwogopa Morrison?

Wanashindwa kuiongoza Yanga? Kama ndivyo, kwa nini waligombea nafasi walizo nazo? Nawashauri wajiuzulu kwa heshima na taadhima badala ya kusubiri kutimuliwa kwa fedheha!

Siku Yanga (au GSM?) ilipotiliana saini mkataba na timu ya Hispania, GSM ndio iliyoonekana kuwa wenye Yanga! Matangazo yote yaliyotolewa jukwaani yalifanywa na mwakilishi wa kampuni ya GSM huku viongozi wa Yanga wakiwa wasikilizaji kama waalikwa wengine.

Walikuwa wakikodoa (kitendo cha kufumbua macho na kutazama kitu kwa muda mrefu) muda wote wa matangazo!

Kulikoni? Au maji yamezidi unga kwa viongozi wa Yanga? Natahadharisha tu kwani ilisemwa "Bora kupigwa dhoruba ya dhahiri kuliko ya siri."

**marobarnabas@yahoo.com**
**0784 334 096**

# TANGAZO

## BUGANDO MEDICAL CENTRE

Consultant and Teaching Hospital

### ADVERTISEMENT FOR

### TENDER OPPORTUNITY FOR SUPPLY & INSTALLATION OF DIGITAL FLUOROSCOPY X-RAY MACHINE AT BUGANDO MEDICAL CENTRE

**Invitation for Tenders**

**Date: 18th July, 2020**

1. The Bugando Medical Centre intends to apply part of its own source of funds towards the cost of Supply and Installation of Digital Fluoroscope X-Ray machine and it intends to apply part of the proceeds of this income to cover eligible payments under the contract for Supply and Installation of Digital Fluoroscope X-Ray machine.

2. The Bugando Medical Centre now invites sealed Tenders from eligible local supplier and who specialized in supply and installation of heavy and automated diagnostics equipment e.g. X-Ray, MRI, CT-Scanner etc who will managed to supply and installation of the named machine with the following option at BMC by payment by installment

3. Tendering will be conducted through the National Competitive Tendering procedures specified in the Public Procurement (Regulations, 2013 – Government Notice No. 446 and is open to all Tenderers as defined in the Regulations.

4. Interested eligible Tenderers may obtain further information from and inspect the Tendering Documents at the office of the ***Secretary of BMC tender board H4 Block P.O BOX 1370 Mwanza from 7:30 am to 15:30 pm local time*** on Mondays to Fridays inclusive except on public holidays.

5. A complete set of Tendering Documents in English and additional sets may be purchased by interested Tenderers on the submission of a written application to the address given under paragraph 4 above and upon payment of a non-refundable fee of **TSH 200,000**. Payment should be by Cash deposit into ***BMC Health Service Fund account no. 01J1051393600 CRDB bank*** and bring original pay slip

6. All Tenders must be accompanied by a Tender Security in the format provided in the Tendering Documents.

7. All Tenders in one original plus two copy, properly filled in, and enclosed in plain envelopes properly written the name of the tender, address, time and the word **"DO NOT OPEN BEFORE"** mentioned time of the deadline and must be delivered to the address ***Secretary of BMC tender board H4 Block P.O BOX 1370 Mwanza*** at or before ***10:00 am local time on*** **31st July, 2020.** Tenders will be opened promptly thereafter in public and in the presence of Tenderers' representatives who choose to attend in the opening at the BMC H4 Conference room Administration Block.

8. Late Tenders, portion of Tenders, electronic Tenders, Tenders not received, and not opened and not read out in public at the Tender opening ceremony shall not be accepted for evaluation irrespective of the circumstances.

**Dr. Fabian Massaga**
**Ag. Director General**
**P.O Box 1370,**
**Mwanza, Tanzania**
**Telephone 2540610/5 or 2500513**
**Fax: 255-028-2500799**
**Email:** info@bugandomedicalcentre.go.tz/ **hospbugando@gmail.com**

## BUGANDO MEDICAL CENTRE

Consultant and Teaching Hospital

### ADVERTISEMENT FOR

### INVITATION FOR SUBMISSION OF TENDER OPPORTUNITY FOR NON-CONSULTANCY SERVICES

**Date: 18th July, 2020**

1. The Bugando Medical Centre has set aside funds towards the cost for the provision of various Non-Consultancy Service and it intends to apply part of the proceeds of this funds towards the payments under the contract for provision of services.

2. The Bugando Medical Centre now invites sealed Tenders from eligible local services providers of various Services as follows;-

   **NON CONSULTANCY SERVICES**

   i. Provision of Catering Services at Bugando Medical Centre Tender no. PA/161/HQ/NC/2020-2021/01

   ii. Provision of Laundry Services at Bugando Medical Centre Tender no. PA/161/HQ/NC/2020-2021/05

3. Tendering will be conducted through the National competitive Tendering (NCT) procedures specified in the Public Procurement (Regulations, 2013 – Government Notice No. 446 and is open to all Tenderers as defined in the Regulations.

4. Interested eligible Tenderers may obtain further information from and inspect the Tendering Documents at the office of the ***Secretary of BMC tender board H4 Block P.O BOX 1370 Mwanza from 7:30 am to 15:30 pm local time*** on Mondays to Fridays inclusive except on public holidays.

5. A complete set of Tendering Documents in English and additional sets may be purchased by interested Tenderers on the submission of a written application to the address given under paragraph 4 above and upon payment of a non-refundable fee of **TSH 100,000**. Payment should be by Cash deposit into ***BMC Health Service Fund account no. 01J1051393600 CRDB bank*** and bring original pay slip

6. All Tenders must be accompanied by a Tender Securing Declaration in the format provided in the Tendering Documents.

7. All applications one original plus **two copy**, properly filled in, and enclosed in plain envelopes properly written the name of the tender, address, time and the word **"DO NOT OPEN BEFORE"** mentioned time of the deadline and must be delivered to the address ***Secretary of BMC tender board H4 Block P.O BOX 1370 Mwanza*** at or before ***10:00 am local time on*** **31st July, 2020.** Applications will be opened promptly thereafter in public and in the presence of Applicants' representatives who choose to attend in the opening at the **Administration Block H4 Conference Hall.**

8. Late applications, portion of applications, electronic applications, applications not received, applications not opened and not read out in public at the tender opening ceremony shall not be accepted for evaluation irrespective of the circumstances.

**Dr. Fabian A. Massaga**
**Ag. Director General**
**P.O Box 1370,**
**Mwanza, Tanzania**
**Telephone 2540610/5 or 2500513**
**Fax: 255-028-2500799**
**Email:** info@bugandomedicalcentre.go.tz/ **hospbugando@gmail.com**

# CCM yataja sababu makada 69 kuwania ubunge Kahama

**Na Neema Sawaka,** KAHAMA

KATIBU wa CCM Wilaya ya Kahama, amesema kasi ya utekelezaji wa Ilani ya chama hicho imewavutia vijana wengi kujitosa kuwania ubunge na udiwani kupitia chama hicho katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka huu.

Emanuely Mbamange amesema uongozi wa Rais John Magufuli umewavutia watu wengi hasa vijana kugombea viti vya ubunge na udiwani kwa kuwa umefanya mambo mengi ya maendeleo kwa muda mfupi.

Kiongozi huyo wa CCM alikuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu mchakato wa uchaguzi huo na mwitikio wa wanachama wa CCM kuchukua fomu za kuwania nafasi mbalimbali.

Alisema kuwa katika orodha ya watia nia waliochukua fomu za kugombea ubunge kwenye majimbo matatu ya Wilaya ya Kahama (Kahama Mjini, Msalala na Ushetu), asilimia 80 ni vijana.

Mbamange alibainisha kuwa, katika Jimbo la Kahama Mjini, hadi kufikia juzi jioni, kulikuwa na makada wa CCM 69 waliokuwa wamejitokeza katika ofisi za CCM kuchukua fomu za kugombea ubunge. Kati yao, wanane ni wanawake.

"Jimbo la Msalala, watia nia waliochukua fomu ni 43, mmoja ni mwanamke na kwa upande wa Ushetu, watia nia ni 17, wanawake ni wawili. Hivyo tuna wanachama 129 waliochukua fomu," alisema.

Jimbo la Kahama Mjini katika Bunge la 11 lilikuwa likiongozwa na Jumanne Kishimba, Msalala lilikuwa chini ya Ezekiel Maige, huku Ushetu likiongozwa na Elias Kwandikwa.




Mwenyekiti wa Mtandao wa Vijana wanaoishi na maambukizi ya virusi vya Ukimwi, Pudensia Mbiliza (katikati), akiwasilisha maombi ya vijana kwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Ajira, Kazi na wenye Ulemavu, .Jenista Mhagama (kulia), kwa niaba ya Waziri Mkuu, ikiwa ni mwitikio wa lengo la kuwasilisha maombi matatu ikiwamo mpango endelevu wa uwezeshwaaji, kiuchumi, kiujuzi na uzalishaji mali kupitia mradi wa 'Hebu Tuyajenge' unaotekelezwa na Baraza la Taifa la Watu wanaoishi na Ukimwi (NACOPHA), na kufadhiliwa na Shirika la Maendeleo la Watu wa Marekani (USAID), jijini Dodoma. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Makada 176 wa CCM wajitosa ubunge Kawe

**Na Waandishi Wetu**

UCHUKUAJI na urejeshaji wa fomu za kuomba kuteuliwa na Chama Cha Mapinduzi (CCM) kuwania ubunge, uwakilishi na udiwani, ulifika kikomo jana jioni, huku makada 176 wakijitosa kulisaka Jimbo la Kawe jijini Dar es Salaam.

Katibu wa CCM Wilaya ya Kinondoni, Sure Mwasanguti, aliiambia Nipashe jijini jana kuwa, makada wa chama hicho waliokuwa wamechukua fomu kugombea ubunge katika majimbo mawili ya wilaya hiyo (Kinondoni na Kawe) walifikia 257 jana, waliwamo 176 walijitosa Kawe.

Mwasanguti alisema baada ya kuona mwitikio mkubwa wa wanachama, waliamua kukutana na watia nia wote, ili kuwaeleza utaratibu wanaotakiwa kuufanya. "Tumekutana na wagombea wote walioomba ridhaa leo (jana) kuwaeleza maadili ya chama na nini wafanye kwa wakati huu wakisubiri hatua nyingine zifuate," alisema.

**WAJIENGUA KONGWA**

Wakati hali ikiwa hivyo wilayani Kinondoni, katika Jimbo la Kongwa mkoani Dodoma, makada 13 walijitokeza kuchukua fomu za kuwania ubunge wa jimbo hilo, akiwamo Spika wa Bunge, Job Ndugai, lakini wanane ndiyo waliorejesha.

Katika Jimbo la Chemba, wanachama 36 walichukua na kurejesha fomu za kuomba kuwania ubunge, huku Jimbo la Kondoa likiwavutia makada 15 waliochukua fomu, huku 11 wakirejesha fomu.

## Vyama vyashauriwa ukomo viti maalum

**Na Joseph Mwendapole**

VYAMA vya siasa vimeshauriwa kuweka ukomo wa viti maalum ili kuwawezesha wanawake wanaopata viti hivyo kwenda majimboni na kuwaachia wanasiasa wengine wapate uzoefu.

Ushauri huo ulitolewa juzi jijini Dar es Salaam na Mwenyekiti wa kwanza wa Shirika la Wanawake katika Sheria na Maendeleo Afrika (WiLDAF), Monica Mhoja.

Mhoja alikuwa akizungumza kwenye semina iliyoandaliwa na WiLDAF kwa ushirikiano na African Women Development Fund (AWDF) ili kuwajengea uwezo wakufunzi watakaokwenda kuwafundisha wanawake watakaowania nafasi za uongozi.

Alisema viti hivyo vinapaswa kuwa daraja kwa wabunge kupata uzoefu na kwenda kugombea kwenye majimbo badala ya kukaa muda mrefu hali inayowanyima haki wanawake wengine.

"Ubunge wa viti maalum iwe nafasi ya kumjengea uwezo mwanamke kwenda kupambana majimboni ili wengine wachanga nao wapate nafasi hizo wajenge uzoefu sasa mtu asikae hapo miaka na miaka," alisema Mhoja

Aidha, alishauri kuwa mtu akipata ubunge wa viti maalum awe na ajenda anayoisimamia ili baada ya miaka mitano watu wamuulize alisimamia nini na kama ni ardhi kila akisimama apige kelele kuhusu haki ya kumiliki ardhi.

Mkurugenzi wa WiLDAF, Anna Kulaya, alisema wakufunzi hao watakwenda kuwafundisha wanawake masuala ya usawa wa kijinsia, uongozi na kushiriki kwenye maamuzi.

"Tunawapa elimu wakawafundishe wabunge watarajiwa ili wajue namna bora ya kushiriki kwenye siasa na wanavyoweza kujenga hoja wakiwa kwenye ngazi za maamuzi," alisema.

Alisema miongoni mwa masuala waliyofundishwa ni kuelewa maana ya kampeni na kwanini kampeni ni muhimu kwenye uchaguzi na kuelewa hatua muhimu kwenye kampeni.

ROCK CITY TAKERS LTD

**TANGAZO LA MNADA WA HADHARA**

**SHAURI LA MADAI NO.326/2019**

MWANZA SACCOS……………………………..MDAI
DHIDI YA
SILVESTER MICHAEL MARWA ………MDAIWA

KWA IDHINI NA MAMLAKA TULIYOPEWA NA MAHAKAMA YA WILAYA YA NYAMAGANA TUTAUZA KWA MNADA WA HADHARA MALI YA MDAIWA AMBAYO NI NYUMBA SIKU YA ALHAMISI TAREHE 06/08/2020 KUANZIA SAA SITA MCHANA NA KUENDELEA. MNADA UTAFANYIKA MAHALA MALI ILIYOKO.

| SN | MALI INAYOUZWA | MAHALI | MUDA |
|---|---|---|---|
| 1 | NYUMBA PLOT NA.320 KITALU "FF" | MECCO KUSINI – MWANZA. | SAA 6 MCHANA NA KUENDELEA |

MASHARTI YA MNADA:
1. MTEJA ATALIPA ASILIMIA ISHIRINI NA TANO YA BEI ITAKAYOFIKIWA KWENYE MNADA NA ITAKAYOSALIA ATAILIPA NDANI YA SIKU KUMI NA NNE,KUSHINDWA KUFANYA HIVYO MTEJA ATAKUA AMEPOTEZA HAKI YAKE YA MSINGI NA MNADA UTARUDIWA TENA.
2. GHARAMA ZOTE ZITAKAZOJITOKEZA BAADA YA KUNUNUA MALI KWENYE MNDA NI JUU YA MNUNUZI.

MAWASILIANO:
0627672221/0659570570

158164

SUMAJKT AUCTION MART COMPANY LIMITED

SUMAJKT AUCTION MART
Efficiency and Excellence

**TANGAZO LA MNADA WA HADHARA**

Kwa idhini tuliyopewa na Tujijenge Tanzania Limited, Suma JKT Auction Mart Ltd tutauza kwa mnada wa hadhara Kiwanja cha wadaiwa sugu kama ilivyoonesha kwenye jedwali. Muda ni kuanzia saa nne Asubuhi.

| JINA LA MDAIWA | JINA LA MWENYE MALI | TAREHE YA MNADA | DHAMANA NA MAHALI ILIPO |
|---|---|---|---|
| Najat Davis Mkony | Jane Dungumaro Hagu - Mdhamini | 01/08/2020 | Kiwanja chenye **Title Deed,** Plot no. 166, Kitalu "I" BUNJU, Wilaya ya Kinondoni |

MASHARTI YA MNADA
Mnunuzi atalipa 25% siku ya mnada na 75% atalipa ndani ya siku 14, akishindwa kulipa salio halirudishwi na mnada utarudiwa tena. Gharama za kubadili umiliki ni juu ya mnunuzi.

Mawasiliano piga:-
SUMAJKT AUCTION MART
0716004554/0753063481
Barua Pepe sumajktauction@gmail.com

158162

**KUPOTEA KWA VYETI**



**Queen Jamhury Kaundama** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba S0448-0029 kilichotolewa na Baraza la Mithihani Tanzania mwaka 2016 katika shule ya Sekondari Sadani na cheti cha Veta chenye namba 245559 kilichotolewa ana Veta Iringa (IRVTSC) mwaka 2017 na cheti cha Kuzaliwa, Cheti cha Darasa la Saba, Kitambulisho cha JKT na Cha Mpiga kura.

**Yeyote atakaeviona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.**

**Polisi Taarifa:**
**OB/RB/2474/2020**

115815702



# Jafo atoa angalizo matumizi bil. 170/-

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, (TAMISEMI), Selemani Jafo, amewataka wakuu wa mikoa, wilaya na makatibu tawala wa mikoa na wilaya kuhakikisha wanasimamia Sh. bilioni 170 zilizopelekwa katika mamlaka za serikali za mitaa kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya elimu. Jafo alitoa agizo hilo jana alipozungumza na viongozi waliteuliwa na Rais John Magufuli hivi karibuni na kuwakabidhi vitendea kazi na miongozo ya majukumu yao kikamilifu katika maeneo yao.

Alisema viongozi hao wana wajibu wa kusimamia fedha za miradi zinazopelekwa na serikali kwenye maeneo yao.

Waziri huyo pia aliwahimiza viongozi hao kuimarisha usimamizi wa mapato na kuhakikisha yanafika katika mfuko wa serikali na siyo vinginevyo.

"Hakikisheni watu wanaocheza na mifumo ya mapato kwa kukwepesha mapato yasiingie katika mfuko wa serikali, wanachukuliwa hatua haraka sana kwani huo ni ubadhirifu," aliagiza.

"Ili kufanikiwa katika utendaji wenu, lazima kuwa na mawasiliano mazuri na watendaji wenu, kufanya kazi kwa muda maalum na kufuata kanuni, taratibu na sheria zilizopo katika kutimiza majukumu yenu, ili kuhakikisha mnaleta utendaji mzuri katika maeneo ya kazi," aliongeza. Sambamba na hilo, aliwataka viongozi hao kuheshimu mipaka ya majukumu yao na kuwa na ushirikiano wa kutosha kwa kila ngazi ili kuleta ufanisi katika utendaji kazi wao.

"Unapokuwa kiongozi, siyo lazima wewe uwe bora peke yako. Hata watendaji wako wanatakiwa kutengenezwa na wao kuwa bora, ili kuleta chachu ya kuwa na watendaji bora nchini na kwa kufanya hivyo katika utendaji wenu, mtakuwa mmeacha alama kubwa katika taifa hili," alisema. Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Joseph Nyamuhanga, aliwataka viongozi hao kufanya kazi kwa bidii, na kufuata sheria, ili kuleta ufanisi katika utendaji wao.

"Jukumu kubwa kwenu ni kusimamia mapato katika maeneo yenu na kuwa na matumizi mazuri ya ofisi na nafasi zenu kwani mmepewa dhamana na mheshimiwa Rais," alisema.

Mkuu mpya wa Mkoa wa Dar es Salaam, Aboubakari Kunenge, alimhakikishia waziri huyo kuwa hawatamwangusha Rais Magufuli kwenye utendaji wao.



Baadhi ya wafanyabiashara wadogo, wakisubiri wateja pembezoni mwa barabara Mtaa wa Mji Mpya, jijini Dodoma jana. Kutokana na changamoto za maeneo maalum ya kufanyia biashara wafanyabiashara hao wamejikuta wakifanyia shughuli zao katika maeneo hatarishi. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# SIDO yamwaga mamilioni kwa wajasiriamali

**Na Peter Mkwavila,**

DODOMA

SHIRIKA la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO) Mkoa wa Dodoma, limetoa Sh. milioni 281.5 kwa watu 156 mwaka wa fedha uliopita.

Justine Kahemela, Ofisa Mikopo wa SIDO Mkoa wa Dodoma, alisema jana kuwa katika mikopo hiyo, viwanda vidogo vinane vimenufaika na kutoa ajira kwa wananchi mbalimbali.

Alisema walionufaika ni wanaojishughulisha katika sekta za viwanda vidogo, kilimo na ufugaji.

Ofisa Mikopo huyo alitoa rai kwa wajasiriamali wa Dodoma kuchangamkia fursa ya uwapo wa mpango wa uendelezaji wa viwanda vidogo na vya kati kupitia mikopo ya kuanzia Sh. milioni nane hadi milioni 500 kutegemeana na uwezo wa mradi.

Alisema kuna mpango ambao unatekelezwa na taasisi tano ambazo ni SIDO, VETA, Benki ya AZANIA, Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii (NSSF) na Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEEC), ukilenga kuwawezesha wajasiriamali wadogo na wa kati kupata mikopo.

"Mikopo iliyotolewa kwa wananchi, takwimu zetu zinaonyesha imekuza miradi yao na imetengeneza ajira rasmi 128 za moja kwa moja, imeongeza kipato na kusaidia wajasiriamali kukidhi mahitaji yao ya kila siku kama vile kuwasomesha watoto na kupunguza kiwango cha umaskini," alisema.

Vilevile, aliwataka wananchi kuendelea kutumia huduma za wataalamu wa shirika hilo waliobobea kwenye teknolojia na viwanda, mafunzo ya uanzishaji na uendelezaji wa biashara, masoko na uwekezaji pamoja na masuala ya fedha.

Ofisa Maendeleo ya Biashara Mkoa wa Dodoma, Crispin Kapinga, alisema fursa za kufanya biashara kwenye mkoa huo ni nyingi na kuwataka wananchi kuzitumia vizuri kujiletea maendeleo.

Meneja wa SIDO Mkoa wa Dodoma, Sempeho Manongi, alisema wanaendelea kuhamasisha wananchi kutumia shirika hilo kutambua fursa zilizopo na kuzalisha bidhaa zenye ubora.

# Ukwepaji kodi kikwazo kwa upatikanaji huduma za msingi

**Na Augusta Njoji, CHAMWINO**

MENEJA Miradi ya Elimu katika Shirika Lisilo la Kiserikali la ActionAid Tanzania, ameitaka jamii kuacha kukwepa kulipa kodi, ili kusaidia upatikanaji wa huduma za msingi ikiwamo ujenzi wa miundombinu ya elimu.

Karoli Kadeghe alitoa rai hiyo jana katika mkutano wa wadau uliokuwa mahsusi kujadili hali ya upatikanaji wa elimu jumuishi katika Wilaya ya Chamwino kupitia Mradi wa Elimu unaoitwa Kuondoa Vikwazo, Haki Kodi na Huduma za Jamii Zinazozingatia Jinsia na Mahitaji Maalum, unaofadhiliwa na Shirika la Maendeleo la Norad.

"Kwa mfano, tunaposafiri tunanunua chakula na watu, hatudai risiti na usipodai ina maana umemwachia fedha za kodi mwenye hoteli na hatawasilisha serikalini. Pia tufuatilie kodi yetu imefanya nini, hasa kwenye huduma za msingi kama elimu, afya na maji," alisema.


Meneja huyo alisema baadhi ya shule bado zina uhaba wa vyumba vya madarasa, hivyo wanafunzi kusomea chini ya miti, akisisitiza kuwa jamii ina wajibu wa kuisaidia serikali kuhakikisha inapata mapato ya kutosha na kufuatilia kwa kina matumizi ya kodi zao. "Tungependa kuona wanajamii wanafuatilia fedha za serikali ambazo ni fedha zao zinazotumwa kwenye shule ili kutimiza malengo yaliyokusudiwa kwa ajili ya utoaji wa elimu," alisema. Alisema kupitia mradi huo, kamati za shule na wazazi wamekuwa na mwamko wa kufuatilia madarasa yanajengwa, ili kuondokana na adha ya watoto kusoma chini ya mti.

"Pale Shule ya Msingi Mahama walikuwa wanasomea chini ya mti, kwa sasa vimejengwa vyumba vitatu, inaonyesha kamati za shule zimetimiza wajibu wake wa kufikisha changamoto zilizopo shuleni kwa viongozi wa kijiji na wengine kwa ajili ya kuchukua hatua," alisifu. Alisema baadhi ya shule zimeweka vyumba kwa ajili ya watoto wa kike kujisitiri wanapokuwa kwenye siku zao, ili wasikose masomo yao.

Akizungumzia kuhusu mradi huo, alisema ulianza kutekelezwa Julai 2018 katika Wilaya ya Chamwino mkoani Dodoma na Mkoa wa Singida kwa shule za msingi 17 na tatu za sekondari na unatarajiwa kukamilika Desemba mwakani, ukigharimu Sh. bilioni 1.4.

Alisema lengo la mradi huo kuwa ni kuondoa vikwazo kwa watoto wa kike na wenye mahitaji maalum, ili wote wafikie fursa sawa ya kupata elimu bora na jumuishi.

"Tunafanya kazi na kamati za shule kwa kuwajengea uwezo wa wajibu na majukumu yao kama wasimamizi ubora wa elimu walipo karibu na jamii, na pia tunafanya kazi na klabu za watoto shuleni wajue haki zao za msingi hasa ya kupata elimu bora," alisema.





# Watalii 270 watua Zanzibar

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WATALII 273 waliingia nchini mwezi uliopita baada ya sekta hiyo kuanza kurejea kufuatia kupungua kwa maambukizi ya corona na kurejeshwa kwa huduma za usafiri wa anga.

Mtakwimu Kitengo cha Utalii Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Raya Mohammed Mahfoudh, aliyasema hayo jana alipowasilisha takwimu za uingiaji wa wageni nchini.

*Alisema idadi hiyo ya wageni imeongezeka kulinganishwa na wageni 173 walioingia Zanzabar Mei mwaka huu.

Alibainisha kuwa asilimia 48.4 ya wageni hao walitoka Ulaya. Alisema asilimia 52 ya wageni hao walipitia Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume na asilimia 48 walipitia bandarini.

Alisema asilimia 52.4 ya wageni ni wanaume na 47.6 ni wanawake ambapo asilimia 3.3 ya wageni hao walikuwa chini ya umri wa miaka 15, asilimia 93.8 wenye umri wa miaka 15/64 na asilimia 2.9 ni wenye umri wa kuanzia miaka 65.

"Wageni hao walitegemewa kukaa kwa wastani wa siku nane," alisema Mahfoudh.

Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar (SUZA), Dk. Stella Ngoma, alisema kurejea kwa sekta ya utalii ni faraja kwa maendeleo ya uchumi wa Zanzibar baada ya zuio la karibu miezi minne lililosababisha sekta hiyo kuyumba kwa kiasi kikubwa.

Alisema hali inaweza kuwa nzuri zaidi baada ya hali kutengemaa Italia ikizingatiwa ndiyo inayotoa idadi kubwa ya wageni wanaoingia Zanzibar.

Hata hivyo, mtaalamu huyo wa uchumi alisema hali ya uchumi wa dunia, itaendelea kukumbwa na mtikisiko kwa miaka kadhaa baada ya janga la corona na Zanzibar itakuwa sehemu ya baa hilo.



Katibu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Wilaya ya kichama Amani, Ali Salum (kushoto), akipokea fedha shilingi laki moja kutoka kwa mwanachama wa CCM Mariyam Ame, alipofika kuchukua fomu ya kugombea Uwakilishi Jimbo la Shauri Moyo, Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Waandishi 14 wagombea majimbo, kata ZNZ

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAKATI mchakato wa Uchaguzi Mkuu wa mwaka huu ukiendelea kupamba moto maeneo mbalimbali nchini, waandishi wa habari 14 visiwani Zanzibar, wamejitokeza kuomba ridhaa ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) kupeperusha bendera ya chama hicho kusaka uwakilishi, ubunge na udiwani.

Kati ya waandishi wa habari hao, wanawake ni 12 ambao wamesema wameamua kugombea nafasi hizo baada ya kuona ushiriki mdogo wa wanawake katika kugombea majimboni uchaguzi uliopita.

Raya Hamad, Ofisa Habari wa Wizara ya Katiba na Sheria Zanzibar, ni miongoni mwa waandishi wa habari waliochukua fomu kuomba kugombea Ubunge Jimbo la Mwanakwerekwe.

Mwandishi huyo aliiambia Nipashe jana kuwa amechukua uamuzi huo ili kuwaleta maendeleo wananchi wa jimbo hilo na kupigania haki za wanawake na watoto.

"Endapo nitapata ridhaa katika chama changu na kisha kuchaguliwa na wananchi kuwa mbunge wao, nitahakikisha ninapigania haki za wanawake na watoto," alisema.

Mwandishi mwingine ni Mariam Ame, ambaye amechukua fomu kuomba kugombea uwakilishi wa Jimbo la Shauri Moyo, akisisitiza kuwa amesukumwa na shauku ya kutaka usawa wa 50 kwa 50 katika vyombo vya uamuzi.

Alisema ni haki yake ya kikatiba kugombea nafasi hiyo pia baada ya kuhamasishwa wanawake kugombea nafasi za uongozi, ameona kuna haja ya kuitikia wito.

"Uongozi wetu wa CCM akiwamo Mwenyekiti wa CCM, Dk. John Magufuli na Makamu wake, Dk. Ali Mohamed Shein, umetujengea imani ya kuweza kugombea. Ukweli na uwazi umeboreshwa ndani ya chama," alisema Mariam ambae ni Mwandishi wa Habari wa Shirika la Utangazaji Zanzibar.

Alisema kwa muda mrefu wanaume wamekuwa wakishikilia nafasi za uongozi, hivyo ameamua kugombea nafasi hiyo.

Suzan Kunambi, mwandishi mwingine kutoka Shirika la Utangazaji Zanzibar, alimechukua fomu kuomba kuwania ubunge Mpendae, akisema ametumia haki yake ya kikatiba na kidemokrasia, ili kuwaletea maendeleo wananchi wa jimbo hilo.

"Chama Cha Mapinduzi ni chama kinachofuata misingi ya demokrasia hata viongozi wetu wamekuwa wakisisitiza kila mwenye sifa kugombea nafasi za uongozi majimboni kwa sababu hakuna milki ya mtu katika majimbo ya uchaguzi," alisema.

Kwa ujumla, waandishi wa habari waliochukua fomu ya kugombea ubunge ni watano, uwakilishi wawili na udiwani wanne na viti maalum watatu.

Mkurugenzi wa Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA), Dk. Mzuri Issa, alisema uamuzi huo ni hatua nzuri na jitihada za wadau kuhamasisha wanawake kugombea zimezaa matunda.

# Wakongwe wajitosa Uchaguzi Mkuu 2020

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

LICHA ya sura mpya hasa za vijana kujitokeza kugombea nafasi za ubunge na uwakilishi kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM), wanasiasa wakongwe waliopata kuwa wabunge kwa zaidi ya miaka 10, wamejitokeza tena kuwania nafasi hizo.

Aliyekuwa mbunge wa Kikwajuni kwa vipindi viwili kuanzia mwaka 2000 hadi 2010, Parmukh Singh Hoogan, ni miongoni mwa wanasiasa wakongwe waliojitosa kuchukua fomu kuwania nafasi ya ubunge jimbo hilo. Hoogan aliiambia Nipashe jana kuwa amevutiwa na mazingira mazuri yaliopo ndani ya CCM yaliyotawaliwa na uwazi na demokrasia aliyoiita 'iliyotukuka'.

Alisema katika kipindi cha uongozi wa Mwenyekiti wa chama hicho, Rais John Magufuli, CCM imekuwa imara ikiwavutia wananchi wengi hadi wapinzani huku rushwa na ubadhirifu zimekomeshwa.


"Nimeamua kuchukua fomu kuomba ridhaa kuwania nafasi ya ubunge kwa tiketi ya CCM baada ya kuridhishwa na mazingira ya uwazi na mapambano ya rushwa yaliyofanyiwa kazi na Mwenyekiti wetu, Rais Magufuli," alisema.

Aliyekuwa mwakilishi wa Makunduchi ambaye ni Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Haroun Ali Suleiman, pia amechukua fomu kuwania tena nafasi ya uwakilishi, aliyoitumikia kwa miaka 20 tangu mwaka 2000. Baada ya kukabidhiwa fomu hiyo katika Ofisi ya Wilaya ya Kusini Unguja, Suleiman ametia nia kuwania nafasi ya uwakilishi, ili kuendelea na mikakati ya kusaidia maendeleo kwa wananchi wa jimbo hilo. Mkongwe mwingine katika siasa za Zanzibar, Dk. Mwinyihaji Makame, pia amechukua fomu ya kuomba kuteuliwa kuwania uwakilishi wa Dimani, jimbo alililoliongoza kwa miaka 20 kuanzia mwaka 2000 hadi sasa.

Mwanasiasa mwingine mkongwe Ussi Yahya, pia ameomba kugombea Jimbo la Mkwajuni kwa kipindi cha pili. Mwaka 1995 alikuwa Mbunge wa Chaani hadi mwaka 2010 na mwaka 2015 aligombea Uwakilishi wa Mkwajuni na kushinda nafasi hiyo.







## MTIHANI MZITO

# Zuchu amsusa baba mzazi, kupanda jukwaani na mama' ake

WAKATI msanii wa kike wa Bongo Fleva, Zuchu, leo anapanda jukwaani kwa ajili ya kuwashukuru mashabiki zake baada ya kumpokea vizuri katika muda mfupi tangu alipotambulishwa.

Bahati mbaya katika shoo yake hiyo itakayofanyika Mlimani City, haikutajwa kama baba yake mzazi atakuwapo kushuhudia binti yake akionyesha kipaji chake cha kuimba.

Hata hivyo mama yake mzazi ambaye ni mwimbaji mkongwe wa taarab nchini, Khadija Kopa, atasimama pembeni ya Zuchu, kumuunga mkono pamoja na kuimba naye baadhi ya nyimbo zake.

Watu wengi wanajiuliza ni nani baba mzazi wa Zuchu? Na inakuwaje hatajwi katika safari ya mafanikio ya mwimbaji huyo chipukizi anayeng'ara kwa sasa?

Maswali hayo yanajibiwa na Kopa mwenyewe wakati akizungumza na radio moja, ambaye amesema Zuchu, ni mtoto halali wa mwimbaji wa zamani wa muziki taarab, Ustaadh Othman Soud.

Ustaadh Othman Soud na Khadija Kopa, wanajuana tangu Zanzibar Culture Music kama mtunzi wake wa nyimbo, kasha wote wakajiunga na kundi Tanzania One Theatre (TOT).

Katika ndoa yao walimpata binti yao huyo na walimuita jina la Zuhura.

Kwa sasa Ustaadh Soud, amerudisha makazi yake Zanzibar, huko anaendelea na harakati zake mbalimbali zinazompatia riziki.

Kulingana na Khadija, jina la baba yake kutotajwa katika safari ya muziki wa Zuchu, inatokana na kutokuwa na ukaribu na mtoto wake.

"Hakuna anayekataa kujulikana baba yake Zuchu, huyo binti yangu anaitwa Zuhura Othman Soud, ni mtoto wake halali, lakini yeye mwenyewe alirudi nyuma katika malezi kiasi ambacho imekuwa vigumu kujulikana," amesema Kopa.

Kopa anasema alifanya juhudi ya kuwaweka pamoja baba na mtoto, lakini mzazi mwenzake hakuonekana kuwa na mapenzi na hivyo Zuchu aliamua kukaa na mama yake.

"Mimi ndiye nilimlea na kumsomesha katika hatua mbalimbali, sikuulizwa jambo lolote wala kupata msaada hadi mwanangu anafikia hatua hii. Siwezi kuweka chuki kati ya mtoto na baba yake, lakini Zuchu alijitahidi kujiweka karibu lakini hakufanikiwa na kuamua kukaa chini," Kopa ameongeza kusema.

BASI SAWA

## Dokii kumfichua mafichoni Rich Mavoko

MSANII nyota wa muziki na filamu, Dokii, amesema kaka yake, Rich Mavoko, yupo salama na ukimya wake utazaa jambo zito litakalowashtua watu wengi.

Akizungumza na EATV, Dokii, amesema anamshukuru mwanamuziki mwenzake Harmonize, kuonyesha nia ya kumsaidia kimuziki.

"Hata kama haonekani wamuache atulie, kama kuna tatizo wao watamsaidia nini? Waache wakisikia tatizo kuhusu Mavoko ndiyo waniulize, ila kwa sasa kila kitu kipo sawa, waache wawe na shauku ya kumuona hadi pale atakapotoka ".



## Kumbe Haitham anabaniwa hivi hivi!

MSANII wa kundi la 'MOCO' Moni Centrozone, amempa ushauri msanii mwenzake wa Bongo Fleva, Haitham Kim, kuwa mvumilivu kutokana na ngoma zake kususiwa na Madj.

Akizungumza katika kipindi cha Friday Night Live (FNL), Moni alimwambia Haitham kuwa watangazaji wengi huwa na tabia ya kuwabania wasanii wa kike, lakini asikate tamaa kwani anatakiwa kufanya kazi nzuri ili iweze kupenya.

"Nikuambie kitu kimoja, Haitham, dawa ya watu kama hao ambao hawatoi sapoti kwenu ni kutoa ngoma kali itapenya tu. Jitahidi kutafuta kitu kizuri na mandhari ya video yako", amesema Moni.





## Ndaro aanza safari ya ubunge Musoma Vijijini

MWIGIZAJI na mtayarishaji wa filamu za Bongo Muvi, Masogo Ndaro, maarufu 'Model' amechukua fomu ya kugombea ubunge wa Jimbo la Musoma Vijijini.

Msanii huyo amekuwa miongoni mwa wanachama zaidi ya 30 wa CCM, waliojitokeza kuwania nafasi hiyo ambayo ilishikiliwa na Prof. Sospeter Muhongo.

Akizungumza na BT baada ya kuijaza na kurejesha katika ofisi ya CCM, Ndaro amesema yeye kijana anayetokana na chama hicho, ana haki ya kutoa mchango wake wa kuwatumikia wananchi kwa kupitia nafasi hiyo.

"Mimi ni kijana niliyekuzwa na CCM kwa muda mrefu, nina haki ya kuomba nafasi mbalimbali kwa ajili ya kuwatumikia wananchi wangu, ubunge naona ndiyo sehemu sahihi ninayoweza kuwaonyesha baba, mama na ndugu zangu wa Musoma Vijijini kwamba ninaweza," amesema.

## Chini ya Jua: Nje malaika, ndani shetani

**Na Adam Fungamwango**

KUNA baadhi ya watu ukiwaona kwa macho ya kawaida tu, unaweza kudhani kuwa ni wema na wacha Mungu.

Lakini nyuma ya pazi wamebeba vitu vizito ambavyo huambatana na wanyama, makatili na kila aina ya uzandiki.

Filamu ya 'Chini ya Jua' imebeba ujumbe mzito ambao unakuwa ni fundisho kwa watu wenye tabia kama hizo.

Kundi la watu wasiojulikana walikuwa wakimuua binti mmoja ambaye ni denti wa chuo. Binti mwingine wa chuo aitwaye Ritha alikuwa akipita porini ambapo ndiyo njia ya kuelekea chuo na kukuta mwenzake 'ametaitiwa' kwa wauaji hao. Akachukua kamera kutaka kupiga tukio hilo. Kwa sababu ni mtoto wa kike, alishindwa kuvumilia kuona denti mwenzake anauawa, akapiga kelele, kamera ikaanguka chini, akakimbia.

Baada ya kuua, watu hao wakaanza kumkimbiza mtu ambaye alipiga kelele. Jitihada zao zilifanikiwa, wakamkatana na kumchimbia shimo refu akamzika ardhini akiwa amesimama wima na kubakisha kichwa tu.

Baada ya mateso makali, wakamuacha hapo wakidhani atakufa. Kijana mmoja wa kijijini aliyeitwa Bahati alipita hapo na kumfukua, akampeleka nyumbani kwake.

Baada ya matibabu, na chakula kwa wiki nzima, hali ya Ritha ikatengemaa.

Rafiki yake Pamela anasambaza ujumbe kwenye magrupu yote na kuanza kusakwa binti huyo ambaye alikuwa akitoka Dar kwenda Tabora chuoni, lakini hakufika na amepotelea kusikojulikana.

Hata hivyo, Pamela huyo huyo naye anauawa na watu wasiojulikana.

Hatimaye baada ya msako wa muda mrefu, Ritha anapatikana. Mwenyewe Ritha baada ya kurejea kwao, anamwambia mama yake kuhusu hali ya kijana Bahati kule kijijini akiwa na mama yake ambaye ni mgonjwa wa akili.

Ritha alitokea kumpenda kijana Bahati, hivyo alijitolea kumtoa kijijini na kumleta mjini, akimtibia pia mama yake hadi akapona.

Baada ya kupona, mama Bahati akakaribishwa nyumbani kwa akina mzee Honchi ambaye ni baba wa Ritha.

Hata hivyo mzee Honchi na mama Bahati wanakataa watoto wake wasioane. Inakuja kudhihirika kuwa ni mtu na dada yake.

Kumbe huko nyuma, mzee Hochi aliwahi kuwa na mahusiano na mama Bahati hadi kumpa mimba, lakini akakataa kwa sababu ana mke tayari. Ndipo alipozaliwa Bahati.

Tukio hilo linawakasirisha wote mle ndani, na kabla chochote hakijaendelea inajulikana kama kumbe pia mzee Honchi ndiye aliyewatuma vijana wasiojulikana kumuua msichana wa chuo ambao nusura pia amtoe roho binti yake Ritha. Ni kwamba msichana yule alitishia kuanika kwa sababu alimpa ujauzito ambao hataki kuulea, hivyo kuficha siri akataka auawe.

Kama vile haitoshi, alipobanwa, mzee Honchi alikiri kuhusika na kifo cha Pamela, ambaye alimuua kwa mkono wake akidhani anaficha siri baada ya kupotea, akidhani kuwa huenda yuko kwa bwana, lakini anajifanya hajui.








## Yasso Boy: Natamani mapinduzi kuboresha sanaa ya mitindo

MWANAMITINDO chipukizi, Yasin Said, maarufu 'Yasso Boy' amesema ugumu wa kupata mianya ya kazi, inasababisha baadhi yao kuvunjika moyo.

Amesema kuna vijana wengi ambao wana ndoto ya kufika mbali kupitia sanaa ya mitindo, lakini wanakwama kutokana na wabunifu kutowaamini.

"Baadhi ya wabunifu wanashindwa kuwaamini wanamitindo chipukizi, lakini kama wangetupa nafasi tungeweza kufika mbali na kuleta ushindani katika tasnia ya mitindo," amesema Yasso.

Aidha, amesema ana ndoto ya kufikia mafanikio ya mwanamitindo Calisah, kwani msanii huyo anampatia changamoto nyingi.

## Tano za Zuchu zinazorindima

**Na Adam Fungamwango**

YOYOTE aliyeangalia Mkutano Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), pamoja na mambo mengine, atakubaliana nami kuwa kwa upande wa burudani, msanii aliyefunika kuliko wote ni Zuchu.

Ni msanii aliyemfanya hata Rais Dk. John Magufuli kutabasamu muda wote anaposikia sauti yake, hasa pale anapoimba ngoma yake ya 'Tanzania Ya Sasa' inayoelezea mambo mbalimbali yaliyofanywa kwenye Utawala wa Awamu ya Tano.

Kwenye Mkutano Mkuu huo, wajumbe walikuwa hawashikiki, wakiserebuka wimbo huo uliotia fora huko Dodoma na nchi nzima waliokuwa wakifuatilia matangazo ya televisheni.

Kwa wale ambao hawamfahamu, Zuchu ni binti wa Malkia wa Mipasho Tanzania, Hadija Kopa.

Kutokana na hali hiyo, wala hauwezi kutumia nguvu au akili nyingi kuhoji kwa nini amekuwa mwimbaji mzuri, mwenye sauti nzuri, lakini kuwa staa kwa kipindi kifupi tu.

Hizi ndizo ngoma tano ambazo zimemfanya Zuchu leo kuzungumziwa nchi nzima.

**Wana**

Ngoma hii inaitwa 'Wana'. Ni moja kati ya ngoma zilizoanza kuwafanya mashabiki wa muziki wa kizazi kipya, kushtuka na kuanza kusikiliza sauti safi za binti huyo.

Ni ngoma ya mapenzi, ambayo binti anamwambia mpenzi wake kuwa penzi ni kidonda, hivyo anamwambia mpenzi ambembeleze, asimpepee ila ampulize, ili mashambenga roho ziwaume.

**Raha**

Ni ngoma ya mapenzi pia. Hapa anasema kuwa anadeka kwa sababu kupendwa raha. Zuchu anaongea maneno mengi ya napenzi ambayo yoyote yule anayependwa na bado hajaanza kupata karaha ya mapenzi anaweza kusema.

Ni moja kati ya ngoma bora kabisa za Zuchu ambazo zimemfanya kufika hapo alipofanikiwa kufika mpaka sasa.

**Kwaru**

Ngoma nyingine ya Zuchu ni 'Kwaru'. Anasema chungu alichopika, wamepakuwa wenzake.

Sasa hii ngoma inaonyesha kabisa kuwa ametendwa. Haya maneno ya mtu ambaye amempenda mtu ambaye hajali hisia zake na mara kwa mara amekuwa wakimkosea heshima kwenye mapenzi.

Mapenzi upende mtu anayejua kuwa huyu mtu ananipenda ili akupende. Lakini akikutana na mtu unayempenda, halafu yeye hajali ni adhabu kubwa.

**Mauzauza.**

'Mauzauza aaa mauzauza. Si wamekushinda kwenu huku kwetu tutakufunza'. Ni moja ya ngoma ambazo zilimtambulisha rasmi. Hii Zuchu ameimba na mama yake mzazi. Na hata mahadhi yake ni kama taarabu hivi, lakini mchanganyiko mkubwa wa mduara.

Hapa mama na binti yake, kila mmoja alionyesha uwezo wa 'kukamua'. Mama akamwonyesha uwezo mtoto na mtoto kamwambia mama kuwa 'mara nyingi vya kurithi huzidi.'

**'Tanzania Ya Sasa'**

Hii ndiyo ngoma ambaye imewachengua wengi kwenye Mkutano Mkuu wa CCM. Ameiimba kwa sauti nyororo, huku ngoma ikiwa na midundo inayofanana na ya 'Kisauzi' hivi.

Ni kama ndiyo wimbo wa nchi kwa sasa, kwani kila kona sasa ukipita, kwenye daladala, mabaa unakutana na ngoma hiyo.






# Kanye West hukujua kusema si kutenda?

WAZARAMO wana msemo wao maarufu, "Zilongwa mbali, Zitendwa mbali" wakimaanisha kusema si kutekeleza kwa jambo. Ndivyo rapa maarufu Kanye West, amejikuta akiinua mikono baada ya kutangaza nia yake ya kuwania urais wa Marekani.

Kanye West, wiki kadhaa amekuwa akitalawa mitandao ya kijamii baada ya kutoa maelezo tofauti kuhusu nia yake hiyo, akisisitiza ni lazima atimize ndoto yake ya kuingia ikulu ya White House.

Hata hivyo kulingana na chama cha Republic, tayari kimemteua Rais Donal Trum, kumalizia muhula wake na hivyo mwanamuziki huyo ametangaziwa hana nafasi ya kuwania kiti hicho.



## Okafor usidharau corona inaua

MWIGIZAJI na mchekeshaji mkongwe wa Nigeria, John Okafor, ambaye anajulikana kama Mr Ibu, amesema hawezi kuamini kama virusi vya corona bado vipo nchini humo.

Akiwa katika mahojiano na chombo kimoja cha habari, msanii huyo amesema hakuna anayeamini kwamba virusi hivyo vimesambaa katika nchi hiyo na hakuna umuhimu wa kuifunga mipaka.

"Wanigeria hatuwezi kuamini kwamba tuna tisho na COVID-19, naona hakuna sababu, kwa nini tuwe katika tisho," amesema.

## Ruth hao ndio wanaume wa Kiafrika

NYOTA wa filamu kutoka Nollywood, Ruth Kadiri, ameamua kuwashauri wanaume wa Kiafrika kuacha kumdhihaki muigizaji wa Marekani, Will Smith, kwa kumsamehe mkewe, Jada Pinkett, baada ya kutoka na mwimbaji August Alsina.

Nyota huyo wa sinema kwenye chapisho lake katika mtandao wa Instagram, amesema idadi kubwa ya wanaume ambao wamemdhihaki Smith, tangu atangaze kumsamehe ni Waafrika.

"Umegundua kuwa wanaume wengi wa Kiafrika walimdhihaki Will Smith, kwa kumsamehe mkewe, unajua ungetamani kuwa na mwanaume anayefanana na huyo, lakini Afrika hilo halipo," ameandika.





## Staa wa Empire matatani kwa kumnyanyasa mke wake

STAA wa muvi ya Empire, Bryshere Gray, amejikuta akiwa matatani baada ya kutuhumiwa kufanya kitendo cha unyanyasaji kwa mkewe.

Mwigizaji huyo, alikamatwa na kufunguliwa mashtaka ya unyanyasaji katika kituo cha polisi cha Arizona, baada ya kupigiwa simu na mke wake.

Tukio hilo lilifanyika majira ya saa 4:15 usiku baada ya polisi kupigiwa simu kutoka kwa kituo kimoja cha kuuza gesi wakiomba kwenda kumwokoa mwanamke mmoja.

## Kifo cha Naya bado kina utata

UTATA bado unaendelea kugubika kifo cha mwigizaji wa Hollywood, Naya Rivera, baada ya mwili wake kuopolewa majini baada ya kuzama katika ziwa moja Kusini mwa California.

Kulingana na mtandao wa PageSix, umesema mwili huo ulionekana Jumatatu ukiwa maili 56 kutoka pwani ya Los Angeles. Katika tukio la kushangaza kulikutwa boti ambalo ndani yake kulikuwa na mtoto wa msanii huyo mwenye umri wa miaka minne.

Kukutwa mwili huo unatokana na kupotea baada ya kuonekana akiendesha boti akiwa na mtoto wake. Mtoto wake huyo Josey, alikutwa amelala ndani ya boti katika Ziwa Piru kwa muda wa saa tatu.

Kanye Wesi hukujua kusema si kutenda?



MAKALA

## KUTOKA SIMIYU...

# Mtihani kutekeleza muda wa ziada shuleni pengo la corona

## ■ Mikasa watoto wadogo, darasani shida

Na Happy Severine

MACHI 17 mwaka huu, serikali ilitangaza kufunga shule zote na vyuo, ikiwa ni hatua zake za awali kupambana na kuenea kwa virusi vinavyosababisha homa kali ya mapafu (COVID-19).

Ni siku moja baada ya mtu wa kwanza kubainika na virusi vya ugonjwa huo. Serikali ilitangaza kufunga shule kwa siku 30.

Baada ya kutimia siku hizo, serikali iliendeleza likizo hiyo, hadi ilipotangaza kufunguliwa, tarehe 29, mwezi uliopita.

Akihutubia bunge jijini Dodoma mwezi uliopita, Rais Dk. John Magufuli, alisema serikali imeamua kufungua shule na vyuo baada ya maambukizi ya ugonjwa kupungua kwa kiasi kikubwa.

Rais anatahadharisha kwamba, bado ugonjwa upo na kuna haja tahadhari zote za kujikinga ziendelee katika mjumuiko shuleni.

Baada ya tangazo, serikali kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ilitoa miongozo ya mihula ya shule na ratiba za mitihani ya taifa inaiyolenga kufidia muda uliopita katika likizo ya corona.

Mojawapo, ilizitaka shule zote za msingi na sekondari kurekebisha ratiba za masomo zilizotumika awali, kabla ya shule kufungwa, kwa kuongeza saa mbili kila siku.

Katika shule za serikali, wanafunzi walitakiwa kuwapo masomoni hadi saa 10:30 jioni, tofauti na mwanzo saa 8.30 mchana.

Mwongozo uliwataka wakuu wa shule na walimu wakuu kuongeza muda kwa wanafunzi wa darasa la tatu hadi la saba, huku darasa la awali hadi la pili wakiendelea na ratiba zilizokuwapo awali.

Sababu zilzotolewa na serikali ni kuwawezesha walimu na wanafunzi kufidia muda wa masomo ulipotea wakati wa likizo ya corona.

**WALIMU NA MABADILIKO**

Tarehe moja mwezi huu, Kamishna wa Elimu katika Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Lyabwene Mtahabwa, kupitia barua yake alizielekeza shule zote nchini kusitisha utekelezaji wa saa mbili za nyongeza, baada ya kubaini kuwapo ugumu wa utekelezaji shule.

Kamishna Mtahabwa, anazitaka shule kuendelea na ratiba za zamani na ndiyo iweze kuamua kama zitaweza kuongeza hizo saa mbili au la, kulingana na mazingira yake.

Kabla serikali kusitisha utekelezaji wa agizo lake la awali la saa mbili, Nipashe lilifanya utafiti wa kuzungumza na walimu, wazazi na wanafunzi kupata uhalisia wa kuongezeka muda.

Wengi walikiri ugumu kutokana na mazingira walio nayo. Charles Yamungu, Mwalimu Mkuu Shule ya Msingi Mhaha, katika Halmashauri ya Mji wa Bariadi, Mkoa wa Simiyu, anakubali lengo la serikali kuongeza muda ni jema, lakini utekelezaji wake ni mgumu.

Yamungu anasema, kwa siku mbili tangu shule kufunguliwa, wanafunzi walipoambiwa muda wa kuondoka shule umeongezeka kutoka saa 8:30 mchana hadi saa 10:00 jioni mengi yalijitokeza.

Anasema, wanafunzi wa madarasa ya tatu, tano na la sita walikutwa na makuu aliyoyasimulia: "Siku ya kwanza baadhi ya wanafunzi wa darasa la tatu walianguka hapa shuleni kutokana na njaa."

Mwalimu huyo anaendelea: "Hawakuzoea kuondoka saa kumi. Sasa limekuja tena ghafla inakuwa ngumu kwao kulimudu.

"Kwa juzi na jana ukiingia darasani saa nane mchana kuendelea na vipindi, hasa darasa la tatu na la tano, unaona wanafunzi walivyo na hali mbaya. Wanakuwa kimya, wengi wamelala, wanaonekana kama hawana nguvu, wanalegea kutokana na njaa."

Mwalimu Rajabu Madaraka wa Shule ya Msingi Gamondo 'A' anasema, inakuwa vigumu kumfundisha mtoto mwenye njaa, kwani uwezo wake wa kusikiliza kile ambacho anafundishwa unakuwa mdogo.

"Inakulazimu mwalimu utafute mbinu nyingine ya ziada kumfundisha mwanafunzi, hasa kumpatia maswali zaidi ili aweze kupata muda wa kuwa huru. Ukimfundisha akiwa na njaa asilimia 90 ya kile ambacho umempatia hakiwezi kuingia," anasema Madaraka.

Adalbert Chambia, Mwalimu Mkuu wa shule, anaendeleza hoja kuwa hata kama wakiamua kuanzisha utaratibu wa kutoa chakula shuleni, utekelezaji wake hautofanikiwa.

"Kuna wazazi hapa wana wanafunzi kuanzia darasa la kwanza hadi la saba. Huyo mzazi hawezi kutoa chakula kwa kila mtoto kukileta hapa, lakini hata mazingira ya kupika ni magumu.

"Kuna gharama za kulipa wapishi, lakini ukipika, itachukua muda mwingi hata wa masomo kuwagawia watoto wote shule nzima," anasema Mwalimu Chambia.

"Kama tumekuwa tunaangaika na wazazi wa watoto wa darasa la nne na la saba walete chakula cha watoto wao, maana wao wanashinda shuleni kutokana na kujiandaa na mitihani, itakuwa ngumu kwa wazazi wote walete chakula shule nzima," anaongeza Chambia.

Mwalimu Mkuu Yamungu, anaeleza ongezeko la muda limeonekana kutowaathiri wanafunzi madarasa nne na saba, kutokana na kuzoea utaratibu huo tangu zamani wakipata chakula shuleni.

Anasema, kigezo kikuu katika hicho ni madarasa ya mitihani ya taifa na wamezoea kuondoka shuleni saa 12:00 jioni, hivyo ongezeko hilo la moda ni kawaida kwao.



Masanja Masunga, Katibu wa Kamati ya Shule ya Msingi Gamondo A, akitoa ufafanuzi namna wazazi walivyojipanga kutatua tatizo la chakula, baada ya kuongezwa saa za kusoma shuleni. **PICHA: HAPPY SEVERINE**

**WAZAZI**

Wazazi waliohojiwa wanasema utamaduni wao kwa muda mrefu, watoto wao wamekuwa wakipata chakula mara moja kwa siku, kwani anapotoka nyumbani asubuhi hakuna anachopewa kwa ajili ya kula.

"Huku hatuna hata utamaduni wa kumpatia mtoto hela ya kula shuleni, kwani maisha yetu ni magumu sana.

"Mtoto akiondoka asubuhi nyumbani anarudi saa nane mchana anapata chakula, kisha jioni saa mbili anapata chakula cha usiku, hapo ni mpaka kesho tena saa nane mchana," anaeleza Masanja Masunga.

Wazazi hao wanasema kwa mtoto wa darasa la tatu kukaa mpaka saa kumi jioni ni mateso makubwa kwao, kutokana na wengi wanatoka nyumbani asubuhi bila ya kupata kifungua kinywa.

"Huku familia zetu hazina utamaduni wa kuamka asubuhi kumpatia mtoto chochote kama ni chai, uji au kiporo na hata awe darasa la awali.

"Akiamka asubuhi ni kwenda shule kisha anarudi kupata chakula cha mchana. Kwa hiyo, kumuweka hadi jioni mtoto ni hatari," anaeleza Jeremia Sitta.

Elizabert Masunga, Mjumbe wa Kamati ya Shule ya Msingi Gamondo 'A' anajadili mbadala kwamba wanapoamua kutoa chakula kwa shule nzima, ni ngumu kutekeleza, kwani wazazi wengi hawana uwezo wa kumudu gharama.

"Kwa ninavyowajua wananchi wa huku uwezo wa kutoa chakula shule nzima ni mgumu sana. Wengi hawana uwezo kwenye familia zao, lakini wapo wengine ni wagumu katika kutoa michango hiyo," anaeleza Masunga.

**WANAFUNZI**

Wanafunzi wa darasa la saba katika Shule ya Msingi Gamondo 'A' wanasema ongezeko hilo la muda wao wanaliona kuwa kama jambo la kawaida, kwani wamezoea lakini wanakiri muda huo wa nyongeza umekuwa mtihani mzito kwa wadogo zao.

"Kuna wanafunzi wa darasa la tatu na la sita, ambao huwa hawapati chakula shuleni, wao wamezoea kuondoka mapema shuleni, tumewaona jana na juzi hali zao zilikuwa mbaya wapo ambao walianguka kutokana na njaa," anasema Yohana Masunga.

Hata hivyo, serikali imeshasitisha utekelezaji wa agizo la awali.

# GRAND RENEISANCE

# Bwawa linalopiganiwa Ethiopia, Misri

## ■Uwepo wake unaweza kuwa baraka au balaa

**Na Mwandishi Wetu**

TAARIFA za siri ambazo zimewashtua mahasimu wa Ethiopia, ni zile za kuanza kujaza bwawa kubwa la maji ambalo limeibua mvutano mkali na mataifa ya Misri na Sudan.

Kwa mujibu wa taarifa zilizofichuliwa kupitia picha za setilaiti, zinaonyesha kuna dalili bwawa hilo ambalo ni kubwa barani Afrika linalofahamika kama Grand Reneisance, limeanza kujaa maji japo kwa taratibu sana.

Taarifa hizo, zimewashtua viongozi wa nchi za Misri na Sudan, ambao muda mrefu walipinga ujenzi wa bwawa hilo wakidai litasababisha kupungua ujazo wa maji katika mto Nile, ambao ni tegemeo kwa uhai wa nchi hizo.

Viongozi wa Ethiopia, wamepinga taarifa hizo na kudai ni propaganda zinazoendelea ili kufifisha mpango wao wa kuhakikishia raia wao kupata umeme wa uhakika na kwa bei nafuu.

**UVUMILIVU UMEKWISHA**

Pamoja na kufichuliwa kwa taarifa hizo, hali kuvumiliana inaonekana kupungua baada ya wawakilishi wa Misri na wenzao wa Ethiopia, kupeana maneno makali katika mkutano wa usuluhishi.

Hivi karibuni, katika mkutano wa Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa, ilioitishwa kwa ajili ya kuzungumzia bwawa hilo, wawakilishi wa nchi hizo walitoleana maneno makali kila mmoja akitetea maslahi ya nchi yake.

Bwawa hilo lililojengwa katika Mto Nile, lipo karibu na mpaka wa Misri na lina uwezo wa kudhibiti kwa kiasi kikubwa maji yanayoingia nchini humo ambayo yanategemewa sana na watu wa taifa hilo la kaskazini mwa Afrika.



Mfanyakazi wa ujenzi katika bwawa la Grand Reneisance, akiuangalia Mto Nile unaotumika kujaza maji. **PICHA: MTANDAO**

Ujenzi wake utakapokamilika inakisiwa inaweza kuzalisha umeme kwa raia milioni 65 wa Ethiopia, ambao kwa sasa hawana chanzo cha uhakika kupata nishati hiyo.

Ujenzi huo ulioanza 2011, imeleta mvutano mkali kati ya nchi hizo tatu ambzo zinategemea Mto Nile kuendesha maisha yao.

Mwakilishi wa Misri katika mkutano huo, Sameh Shoukry, amesema uwepo wa bwawa hilo linaweza kuingilia maisha ya Wamisri milioni 100, jambo ambalo hawataki litokee.

Balozi wa Ethiopia katika Umoja wa Mataifa, Taye Atske-Selassie alijibu mapigo kwa kusema nchi yake kutumia maji yake sio suala la kuchagua, bali ni jambo la umuhimu.



Bwawa la maji la Grand Renaissance likiwa katika hatua ya ujenzi.

**MZOZO WA KUJAZA MAJI**

Katika mfululizo wa vikao vya usuluhishi, jambo muhimu la kuanza kujaza maji katika bwawa hilo, bado halijapatiwa ufumbuzi.

Nchi zinazopinga, zinataka kuwapo na makubaliano namna ya kujaza na kiwango gani cha maji kinachotakiwa kuchepushwa kuingia ndani ya bwawa.

Katika kipindi hiki cha msimu wa mvua, Ethiopia inasema itaanza kulijaza bwawa hilo katika kipindi cha wiki chache zijazo.

Ili bwawa hilo lijae kama inavyotakiwa inatakiwa kuchukua miaka saba, jambo ambalo ni hatari na inaweza kupunguza kiwango cha maji ya Mto Nile.

**CHANZO CHA PICHA,GETTY IMAGES**

Hata hivyo, mwakilishi wa Ethiopia, anasema hatua ya kulijenga na kulijaza maji bwawa hilo, itakuwa katika nyakati tofauti na si mwaka mmoja.

"Wamisri walijaribu kuwachanganya maofisa wa jamii ya kimataifa kwa kusema kwamba ni mambo tofauti", anasema.

Baada ya Marekani na Benki ya Bunia kuhusishwa mwisho wa mwaka jana, zilishindwa kuishawishi Ethiopia kutia saini hati iliyokubaliwa na Misri mwezi Februari, huku Muungano wa Afrika AU, ukitafuta njia kutafuta suluhu.

Iwapo maneno ya Waziri wa Mambo ya Nje wa Misri yatatiliwa maanani. basi makubaliano yanatakiwa yawe ya haraka.

**UTATA WA MKATABA WA KIKOLONI**

Utata wa umiliki wa maji ya Mto Nile unatokana na mkataba wa mwaka 1929, ambao unaipa Misri haki ya kumiliki mto huo.

Wakati wa serikali ya ukoloni wa Uingereza ilipotambua kuwa haki asilia na zile za kihistoria za Misri kuhusu maji ya Mto Nile.

Pia iliipatia Misri haki ya kufanya mradi wowote kati maji hayo.

Mwaka 1959, Misri na Sudan zilitia saini makubaliano ambapo mataifa hayo mawili kugawana raslimali za mto Nile huku Misri ikichukua maji mengi.

Hakuna taifa jingine lililotajwa kati ya mataifa 9 ambayo maji hayo yanapitia ikiwamo Ethiopia ambayo ndio chanzo cha Mto Blue Nile.

Maji hayo ambayo yanaungana na maji ya Mto White Nile, unaokatisha katikati ya mji mkuu wa Sudan, Khartoum, hutoa karibu asilimia 80 ya mtiririko mzima wa maji ya mto huo.

Ethiopia inaona mkataba huo haujatoa haki na haiwezi kuutii.

"Iwapo Ethiopia itakubali kuachilia kiwango fulani cha maji kuelekea Misri kila mwaka, basi hatua hiyo itathibitisha fursa ya kikoloni inayofurahiwa na taifa kama Misri. Ni kama ukoloni mambo leo na hilo halitakubalika", anaongeza kusema Zerihun. Ethiopia inailaumu Misri kwa kutaka kuendeleza mabavu yake ili kudhibiti maji hayo kwa kutumia fursa ya matumizi waliyopewa mwaka 1929.

Ethiopia inasema kwamba wakati itakapokuwa ikilijaza maji kwenye bwawa hilo kwa mwaka wa pili, itaachilia maji yenye ujazo wa mita bilioni 31 kupitia bwawa hilo, lakini zaidi ya hilo haiwezi kulazimishwa kutoa kiwango fulani.

Usisitizaji wa kuachia kiwango fulani cha maji kwenda Misri, bila kujali iwapo mvua au la, inaweza kusababisha bwawa hilo kutojaa na kufanya kazi wakati wa kiangazi.

Uwepo wa mvutano mkali baada ya miaka tisa ya mazungumzo, huenda ukatoa ukweli kwamba huu ndio mwisho wa kidiplomasia badala ya kuwapo makubaliano.

Lakini viongozi wote wawili wa Misri, Abdula Fattah al Sisi, na Waziri Mkuu wa Ethiopia Abiy Ahmed, wanakabiliwa na shinikizo la kisiasa kutoka kwa raia wao ambao wamejikita kwenye siasa kuhusu suala hilo.

HABARI KIMATAIFA

# Waathirika wa sumu kulipwa fidia

**NAIROBI, Kenya**

JAJI mmoja nchini Kenya, ameamuru kulipwa fidia kiasi cha dola za Marekani milioni 12, kwa watu walioathiriwa na kusambaa kwa sumu ya madini ya risasi.

Hukumu hiyo imetoka baada ya mkazi mmoja wa eneo la Owino Uhuru, mjini Mombasa, Phyllis Omido, kufungua kesi ya kudai fidia baada ya mtoto wake kuathirika na sumu hiyo inayotokana na betri chakavu.

Mtoto wake aliugua baada ya yeye kufanya kazi katika vinu vya kuzalisha madini hayo kwa miezi mitatu.

Baada ya vipimo, madaktari waligundua kuwa alikuwa na sumu mwilini ambayo alipata kwa njia ya kunyonyeshwa na mama yake.

Hata hivyo, ilibainika wakazi wa eneo hilo walikuwa na matatizo ya aina hiyo, na kusababisha kufungwa kwa vinu hivyo mwaka 2014.

Omido alifungua kesi mwaka 2016, akiitaka serikali ilisafishe eneo hilo na kulipa fidia kwa familia za wale waliopoteza maisha au kuugua kutokana na athari za madini hayo. Jaji Ann Omollo, aliamuru pamoja na ulipaji fidia, serikali inatakiwa kuondoa madini yote ya risasi yaliyosalia.

**BBC**



Jengo moja lililoanguka ndani ya maji wakati mafuriko yakiendelea kuathiri mji wa Poyang, ulioko jirani na Ziwa Poyang, nchini China. **(PICHA: AFP)**

# Majasusi Urusi wajaribu kudukua chanjo ya corona

**LONDON, Uingereza**

TAHADHARI imetolewa kuwa kundi la majasusi kutoka Urusi wanalenga kufanya udukuzi kwa kampuni zinazojaribu kutengeneza dawa ya chanjo ya virusi vya corona katika nchi za Uingereza, Marekani na Canada.

Wataalamu kutoka kituo cha masuala ya usalama wa mitandao ya kompyuta, walisema majasusi hao wanafanya kazi hiyo kama sehemu ya watumishi wa idara ya usalama.

Hata hivyo, kituo hicho hakijasema ni kampuni ngapi zinalengwa na wadukuzi hao au kama kuna taarifa zozote zilizoibiwa.

Lakini kituo hicho kilisema utafiti kuhusu chanjo haujaathiriwa na wadukuzi hao.

Urusi imetupilia mbali tuhuma hizo, ikisema haihusiki na tukio hilo. "Hatuna taarifa kuhusu nani aliyedukua kampuni ya dawa na vituo vya utafiti nchini Uingereza. Tunaweza kusema jambo moja, Urusi haihusiki na majaribio ya udukuzi," alisema Dmitry Peskov, msemaji wa Rais Putin.

Tahadhari hiyo ilichapishwa kwenye taasisi za kiusalama za Uingereza, (NCSC), Canada (CSE), Idara ya Usalama wa ndani Marekani (DHS) na Shirika la Usalama wa Miundombinu ya Kimtandao (CISA) pia Idara ya Usalama wa Taifa ya Marekani (NSA).

Mtaalamu mmoja wa masuala ya usalama, alikiri kuwapo kwa mpango huo.

Taasisi hizo zilisema wadukuzi wameharibu programu inayosaidia kufikia mifumo ya kompyuta na walitumia programu za Well Mess na Well Mail kuweka na kupakua makablasha kutoka kwenye mashine zilizoharibiwa.

**BBC**

# Umoja wa Ulaya kujadili bajeti

**BERLIN, Ujerumani**

VIONGOZI wa Umoja wa Ulaya wamekiri kuwa kuna safari ndefu kufikia makubaliano ya bajeti ya euro trilioni 1.85 kusaidia uchumi ulioporomoka kutokana na virusi vya corona.

Utoaji wa fedha hizo utakwenda sambamba na kuanzishwa kwa mfuko maalum wa kufufua uchumi.

Alipowasili katika Baraza la Umoja wa Ulaya, Rais wa Halmashauri ya Umoja wa Ulaya, Ursula von der Leyen, alisema kuna umuhimu kupambana na mgogoro unaowakabili.

"Suluhisho linalotarajiwa kutoka kwetu na watu wa barani Ulaya, kwa sababu ni kazi zao ambazo ziko hatarini na hatari ya virusi bado inaendelea," alisema Vod der Leyen.

Umoja huo unakabiliwa na hali mbaya ya kiuchumi, huku wanachama wake wakizozana kuhusu nani anayestahili kuchangia kiasi kikubwa zaidi cha fedha, na nchi gani zinafaa kupewa kiasi kikubwa cha fedha ili kufufua uchumi.

**DW.**

## Mazungumzo Kosovo, Serbia yaanza tena

**BRUSSELS, Ubelgiji**

VIONGOZI wa nchi za Serbia na Kosovo, wamekutana kwa ajili ya mazungumzo ya ana kwa ana yatakayopunguza mvutano wa pande hizo mbili.

Mkutano huo ulifanyika juzi mjini Brussels, ulishuhudia Serbia ikiishutumu Kosovo kwa kulazimisha masharti yasiyowezekana.

Wiki iliyopita, viongozi hao walizungumza kwa nia njia ya mtandaoni kabla ya maofisa wa Umoja wa Ulaya kuandaa mkutano mwingine wa ana kwa ana.

Rais wa Serbia Aleksandar Vucic na Waziri Mkuu mpya wa Kosovo, Avdullah Hoti, walikutana wakinuia kufufua juhudi za kuimarisha uhusiano wao.

Mkutano huo unajiri baada ya miongo miwili tangu majirani hao wapigane vita na kuacha mvutano unaotishia amani katika eneo hilo.

Mwakilishi maalum wa Umoja wa Ulaya katika mazungumzo hayo, Miroslav Lajcak, alisema mkutano huo unalenga kuwajadili sehemu waliko watu wasiojulikana, waliopoteza makazi pamoja na maendeleo ya kiuchumi.

DW

## Mwandishi ahukumiwa kifungo Uturuki

ANKARA, Uturuki

MAHAKAMA moja ya Uturuki, imemuhukumu mwandishi wa habari maarufu mwenye asili ya Uturuki na Ujerumani Deniz Yucel, kifungo cha miaka mitatu jela kwa kosa la kueneza propaganda za wanamgambo wa Kikurdi.

Yucel mwenye umri wa miaka 46, alisomewa hukumu hiyo wakati yeye hayupo mahakamani analifanyia kazi gazeti la Ujerumani la Die Welt.

Mwandishi huyo alisababisha mvutano kati ya Uturuki na Ujerumani mwaka 2018 baada ya kutumikia kifungo cha mwaka mmoja gerezani.

Yucel alikamatwa baada ya kuripoti habari inayohusu kudukuliwa kwa akaunti ya barua pepe ya waziri wa nishati wakati huo, Berat Albayrak.

**DW**

# HADITHI

# Mauaji Harusini-21

ILISEMWA hapo zamani kuwa dunia inaharibiwa na vitu viwili tu. Mapenzi na mali. Vitu hivi vinaweza kumfanya binadamu aende popote. Afanye chochote kile ili awe navyo, wengine wanakwenda mbali zaidi mpaka ikiwezekana hata kutoa uhai wa wenzao.

Shani, binti wa kitajiri anapitia kwenye mikasa mikubwa mizito ya kupotezwa kwa wazazi wake na kumsababishia ukiwa na mawazo tele.

Wakati ikionekana binti huyo pekee kwa wazazi wake akielekea kurithi utajiri wa wazazi wake, kiu ya damu inaanza kuwaingia baadhi ya ndugu za wazazi wake ili apoteze maisha, wao waweze kumiliki mali hizo.

Hapo ndipo uhai wa Shani unapokuwa matatani na patashika nguo kuchanika inapoanza. Fuatilia mkasa huu kuburudisha, kuelimisha na kusikitisha.

**Na Adam Fungamwango, (0716 350534)**

Kinywaji kilipofika alianza kunywa taratibu, akivuta muda wa kumpokea mgeni wake, ambaye hapo yeye alikuwa ni mwenyeji kuliko anayemsubiria.

Muziki mororo ulitumbuiza kutoka kwenye spika ziliokuwa pembeni. Macho yake yalikuwa yakiangalia kila kitu kilichokuwa humo, mpaka alipojidhihirisha kuwa ni salama kama kawaida yake.

Kulia kwake kulikuwa na meza ya baba mmoja kibonge mtu mzima, aliyekuwa amekaa na mpenzi wake, mithili ya baba na binti yake wa tatu au wa nne.

Kilichomvutia Eddy ni maneno ya mzee huyo aliyokuwa akiyaongea kwenye simu iliyoonekana anaongea na mkewe.

"Nimepata safari ya ghafla mke wangu ya kikazi kwenda Morogoro, yaani leo sitorudi hadi kesho jioni."

Na baada ya kumaliza kuongea, akamgeukia mpenzi wake.

"Kwisha kazi mke keshaingia kingi, yaani leo ni kula bata tu hadi kuku waone wivu. Leo tutalala hapa hapa hotelini hadi kesho jioni."

Eddy alimtupia jicho la wizi, akatabasamu. Wakati huo mhudumu mmoja wa kiume alifika na kuwaongezea vinywaji.

Wakati akiwa wamevuta hatua tano tu, ghafla kuna kitu kilianguka kutoka kwenye mfuko wake kwa bahati mbaya.

Ni Eddy tu ndiye aliyekiona. "Ni leso, au pesa?" Alijiuliza. Haraka akili ikamtuma ajidhihirishe kwanza kabla ya kumwita aje kuchukua kitu alichoangusha.

Aliinuka kama vile anayetaka kwenda msalani, akavuta hatua chache tu, haraka akainama na kuokota kitu kile kabla yeyote yule hajaona.

Akakaa kwenye kiti. Ilikuwa ni kifuko kidogo cha nailoni kilichofunguliwa. Kilikuwa na unga wenye rangi ya kahawia ambao tayari ulikuwa nusu. Akahisi hatari. Akatoa leso mfukoni na kukiweka kifuko kile katikati ya leso yake ili kuzuia unga usitoke na kugusa mikono yake. Akasoma maandishi yaliyo kwenye kifuko hicho.

Akatabasamu. Halikuwa tabasamu halisi. " Hii ni sumu" Alijisemea moyoni.

Katika kazi yake ya upelelezi amekutana na vitu vingi, ikiwamo aina mbalimbali za silaha za moto na za kibaiolojia, ikiwamo sumu mbalimbali. Pia si kwamba tu alipata kuziona, lakini alipata mafunzo ya kujua aina mbalimbali za sumu, zinazoua haraka na zinazoua taratibu.

Haraka alitoka na kwenda msalani. Huko alichofanya ni kuiweka kwenye hali ya usalama zaidi kwa kuifunga vizuri, isije hata yeye mwenyewe ikamletea madhara. Baada ya kuridhika akaiweka kwenye mfuko wa nyuma wa suruali yake. Akarejea sehemu yake na kukaa kama awali.




Robo saa baadaye aliingia msichana ambaye alibadilisha hali ya hewa kwenye ukumbi wa ABC Club.

Sura yake nzuri iliyonyesha dalili zote za umri mdogo wa miaka 23 na hakuzidi hapo.

Alivaa gauni fulani la bluu hivi ambalo si fupi sana na wala si refu, lakini liliacha mapaja yaonekane kwa kiasi fulani.

Nywele ndefu laini zilizozingira sura yake kama bustani nyeusi, ziliwafanya wanaume karibuni wote ndani humo, kuacha stori na wapenzi wao na kuangalia kiumbe kile kwa muda.

Baadhi walifinywa, au kupigwa kofi na wapenzi hao baada ya kuona ni kama wamepumbaa hivi kuangalia mrembo, wakati pale walipo walikuwa na warembo wengine.

Urefu alionao, matiti yaliyoshiba na kukita kufuani, kiuno chembamba kilichokatika kama anavyotaka kila mwanaume, kilimuongezea urembo unahitajika.

Alitoa tamasamu tamu jepesi, akiangalia huku na huko kama anayetafuta kitu.

Kila mwanaume alikuwa akimwangalia mwanaume mwenzake ndani mle, wakionekana wivu, kwani walijua huenda angeenda kukaa kwa mmoja wapo, hasa wale waliokaa peke yao.

Hata hivyo kuna baadhi ya wateja walikuwa wameshamzoea, hivyo waliishia kummezea mate na kuendelea na shughuli zao.

Kamal alimuona mgeni huyo aliyekuwa anaingia. Kwake hakuna mgeni. Alisimama na kunyoosha kidole.

Kitendo hicho kilifanya mgeni wake kumuoa. Taratibu alianza kumfuata, kwa mwendo wa madaha kama twiga, huku kila mmoja ndani ya ukumbi akionekana kufuatilia zoezi lile.

"Karibu Shani."

"Mimi ndiyo nikukaribishe wewe." Alijibu.

"Umefika muda eee."

"Hapana si muda mrefu sana. Nadhani ni dakika kumi na tano zilizopita." Alidanganya.

Kama Shani angemuuliza mtu yoyote aliyemuona Eddy wakati anaingia, angeshangaa jibu ambalo angepewa.

Aliingia humo saa moja na dakika kumi zilizopita. Hakutaka kumwambia ukweli Shani kwa sababu ni lazima angeoshesha mshangao na maswali kadhaa juu yake.

Hata angemjibu kuwa ni sababu za kiintelejensia, au usalama, ingeongeza mshtuko zaidi ya mshangao aliokuwa nao. Na hata angekubaliana na hilo, ni lazima angejiuliza sehemu ya starehe na usalama wapi na wapi?

Hakutaka pia Shani kuanza kumshuku kuwa mwenzake hakuwa na mtu wa kawaida.

Anakumbuka mara ya kwanza alipoongea naye pale makaburini, kuna maneno alimwambia ambayo yalimshtua Shani.

"Usilie. Msichana mdogo, mzuri na mrembo kama wewe hupaswi kulia hapa. Angalia watu waliopita njiani wanakuangalia unavyolia. Mimi mwenyewe nimeumia kutokana na kifo cha shangazi yangu, lakini silii. Mungu anasema umuombe huku na wewe unafanya kazi. Kazi itakayofuata sasa ni kuwasaka wauaji."

"Uwasake wauaji, kwani unawajua?"

"Siwajui?"

"Sasa utawasaka vipi?"

"Kwani wewe unaitwa nani?"

"Naitwa Eddy Kamal"

"Ni askari wewe kwani."

"Hapana, mimi nilikwambia mwanzo nimetoka kusoma Marekani. Kwa sasa sina kazi yoyote ile."

"Uko nyumbani tu?"

"Ndiyo maana yake."

Hayo yalikuwa ni maneno ambayo anakumbuka yalimfanya Shani siku ile kuwa na wasiwasi naye, hivyo kama angewambia ukweli angeweza kuunganishi 'doti'.

"Umeagiza chakula?" Shani aliuliza.

'Nilikuwa nakusubiri ili uagize. Mimi nitakula chakula ambacho wewe utakula."

Shani alitabasamu na uzuri wake ukaongezeka.

Ghafla, kati yao alisimama kijana yule yule ambaye aliangusha kifuko ambacho Eddy aliona kama ni sumu.

Alikuwa amefika pale muda sekunde chache tu baada ya Shani kufika.

"Niiletee chakula changu ninachokipenda." Shani aliamwambia kijana yule ambaye walionekana kuwa wamezoeana.

"Hapana." Eddy aliingilia kati.

"Nimeshaagiza chakula kwa mhudumu mwingine wewe unaweza kuendelea kwenye meza zingine." Aliongea kwa sauti ya upole.

Shani na mhudumu yule ambaye hakuwa mwingine ila ni Fikiri walipatwa na mshangao. Fikiri pamoja na mshangao, lakini pia alishtuka.

*Itaendelea Jumamosi*

HABARI MICHEZO

# SOLSKJAER

## ATAMBA WAKO TAYARI KUWAVAA CHELSEA




**MANCHESTER, England**

OLE Gunnar Solskjaer amesisitiza Manchester United "wapo tayari" kwa ajili ya mchezo wa nusu fainali ya Kombe la FA dhidi ya Chelsea.

Mabao kutoka kwa Marcus Rashford na Anthony Martial yalishuhudia United ikiibuka na ushindi wa magoli 2-0 dhidi ya Crystal Palace kwenye Ligi Kuu England juzi Alhamisi usiku na kuendelea kujiweka kwenye nafasi nzuri ya kumaliza katika nafasi nne za juu.

United hawakupata mapumziko kuelekea mchezo huo dhidi ya Chelsea na Solskjaer alihoji kwanini kikosi cha Frank Lampard kilipewa saa 48 za mapumziko kabla ya mchezo huo wa Jumapili.

Lakini kocha huyo wa United amesema wachezaji wake wapo tayari kwenda katika mchezo dhidi ya Chelsea pale kwenye dimba la Wembley.


"Tuko vizuri, tuko fiti na wachezaji wapo tayari kwenda na wanataka kucheza tena," alisema Solskjaer akiwaambia waandishi wa habari.

"Bila shaka, yoyote anaweza kukumbatia mikono yake kwa sasa na kusema, 'nataka kukaa nje'.

"Ukiwa na wachezaji wapo benchi wanahofia kuingia uwanjani, maana yake wanahofu, lakini kwa upande wetu wachezaji wote wapo tayari kwa ajili ya mchezo unaokuja.

"Ni Brandon (Williams) na Luke (Shaw) ndio hawakuwa tayari, lakini Timothy (Fosu-Mensah) alifanya kazi kubwa na Scott (McTominay), amekuwa kwenye kiwango cha kuvutia. Anapokezana na Nemanja (Matic)."

United wapo nafasi ya tano kwenye msimamo wa Ligi Kuu England, wakipitwa pointi moja na Chelsea ambao wapo sawa na Leicester City iliyopo nafasi ya nne, huku zikiwa zimebakia mechi mbili ili msimu kumalizika.



## CONTE ATARAJIA MAKUBWA KWA ERIKSEN

**MILAN, Italia**

ANTONIO Conte "ameridhishwa" na Christian Eriksen, lakini amekubali kwamba anataka kuona mengi zaidi kutoka kwa mchezaji huyo mara atakapojikita zaidi kwenye maisha yake hapo Inter.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Denmark alirudi kwenye kikosi cha kwanza cha Inter Milan Alhamisi wakati wakiibuka na ushindi wa mabao 4-0 dhidi ya SPAL baada ya kutokea benchi katika mechi mbili zilizopita.

Eriksen amekuwa hana kiwango cha kuvutia na kulikuwa na ripoti kwamba huenda akauzwa mwishoni mwa msimu huu, ikiwa ni miezi sita tangu ajiunge akitokea Tottenham.

Lakini wakati Conte anaamini mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28 anaweza kuimarisha soka lake, ana furaha kwamba tayari ameanza kuimarika tangu alipotua hapo Januari.

"Christian anafanya kazi nzuri, anajaribu kwenda na falsafa ya timu na ligi hiyo ambayo ni ya kiufundi zaidi kuliko ile ya England," alisema Conte akiiambia DAZN.

"Ni mchezaji mwenye ubora ambaye anajaribu kujiimarisha yeye mwenyewe, kuwa na kasi na mbinu kwenye mchezo, ndio kitu ambacho tulikuwa tunataka kutoka kwake."

## PEREZ AFUNGUKA HATIMA YA RAMOS

**MADRID, Hispania**

FLORENTINO Perez ana uhakika Sergio Ramos atamalizia soka lake pale Real Madrid baada ya kuwaongoza kwenye ubingwa wa taji la 34 la LaLiga juzi Alhamisi.

Ushindi wa mabao 2-1 wa Los Blancos 2-1 dhidi ya Villarreal uliwahakikishia ubingwa huo wa kwanza wa Ligi Kuu Hispania tangu msimu wa 2016-17 wakati wakiwa wamelipokonya kombe hilo kutoka kwa wapinzani wao, Barcelona.

Ramos alikuwa na mchango mkubwa kwa kipindi chote cha msimu, akifunga mara tano katika mechi 10 za LaLiga zilizopita.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 34, mkataba wake unamalizika mwishoni mwa msimu unaofuata na alisema angependa kumalizia soka lake Madrid, ingawa alikubali kwamba ilikuwa inategemea na Perez anataka nini. Na sasa rais huyo wa klabu amebainisha anataka Ramos amalize kipindi chake cha kucheza soka akiwa na jezi ya klabu hiyo.

"Ramos kwa uhakika kabisa atamalizia soka lake akiwa na jezi ya Madrid," alisema Perez akiiambia Movistar.

"Ingawa kuna mazungumzo kuhusu hilo, mambo hayatabadilika kila mtu ametulia. Yeye ni zaidi ya nahodha. Ameiongoza timu kwenye mambo mengi mazuri."

# SETIEN:

## SINA UHAKIKA WA KUBAKIA BARCELONA



**BARCELONA, Hispania**

KOCHA Quique Setien amekubali hana uhakika kama ataendelea kuinoa Barcelona kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya mwezi ujao.

Barcelona walipokea kichapo cha mabao 2-1 kutoka kwa Osasuna Alhamisi wakati Real Madrid wakibeba taji la Ligi Kuu Hispania, LaLiga kwa mara ya 34.

Lionel Messi alisema Barca wanahitaji kujitafakari wao wenyewe kama wapo tayari kuivaa Napoli kwenye mchezo wa pili wa Ligi ya Mabingwa Ulaya hatua ya 16 Bora, baada ya mchezo wa kwanza kutoka sare ya 1-1 nchini Italia.

Alipoulizwa kama angependa mchezo dhidi ya vijana wa Gennaro Gattuso ungechelewa kwanza, Setien alijibu: "Natumaini hivyo, lakini sijui.

"Nakubaliana na Messi kuhusu kujitafakari sisi wenyewe."

Wakati Setien bado anaipa nafasi ya Barca kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, lakini akasema majaliwa yake yapo nje ya mikono yake.

"Mimi ndio mhusika mkuu. Ndio mwenye nguvu na ndio kiongozi, bila shaka yoyote, lakini sijui majaliwa yangu," alisema.

"Sishawishiki kama tutakwenda tukiwa timu tofauti, tukiwa na tumejipanga kuingia kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa nguvu na kasi ya juu.

"Hadi wakati huo ndio naweza kusema kitu, lakini kwa sasa mambo yapo nje ya uwezo wangu. Tayari nilishawahi kuishi kwenye hali kama hii."

Tangu msimu wa LaLiga ulivyorudi mwezi uliopita, Barcelona wameshinda mechi sita tu kati ya 10, huku Madrid wakiwa wameshinda zote 10.

## MARTINELLI KUREJEA DIMBANI MWAKANI

**LONDON, England**

ARSENAL imethibitisha kwamba, fowadi wake kinda, Gabriel Martinelli hataweza kurudi kwenye mazoezi hadi mwishoni mwa mwaka huu, baada ya kufanyiwa upasuaji wa goti.

Martinelli alijiunga na Arsenal akitokea klabu ya nchini Brazil ya Ituano mwaka jana na amefunga mabao 10 na katika mechi 26 kabla ya kuumia goti wakati wa mazoezi Juni 21, mwaka huu.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 19, ambaye alisaini mkataba wa muda mrefu wiki mbili zilizopita, awali alitarajiwa kuwa nje ya dimba kwa miezi miwili au mitatu, lakini sasa imebainika hatarudi uwanjani hadi mwishoni mwa mwaka huu.

Taarifa ya Arsenal iliyowekwa kwenye tovuti yake ilisomeka: "Kwa sasa anaendelea kujiuguza goti baada ya kufanyiwa opereshení, ambayo ilifanyika mwishoni mwa Juni.

"Upasujia ulikuwa na mafanikio makubwa, huku timu ya madaktari wetu ikiendelea kumfuatilia kwa karibu katika hatua yake ya kujiuguza.

"Kwa sasa hatakuwa sehemu ya mazoezi kwani anaendelea kuwa chini ya uchunguzi wa madaktari.

"Ataendelea kujiuguza kwa msimu wote hadi mwishoni mwa mwaka huu 2020, ambapo hapo ndio anatarajiwa kurudi uwanjani."



## KANE AZUNGUMZIA MIPANGO YA SPURS

**LONDON, England**

HARRY Kane amewaonya wachezaji wenzake wa Tottenham kwamba kitu chochote nje ya pointi sita katika mechi zao mbili zilizobaki, itawafanya washindwe kufuzu kucheza Ligi ya Europa msimu ujao.

Spurs walipata ushindi wa 3-1 dhidi ya Newcastle United Jumatano na kuwavuta hadi nafasi ya saba kwenye msimamo wa Ligi Kuu England, kitu ambacho kitawawezesha kufuzu kucheza Ligi ya Europa msimu ujao.

Huku Ligi Kuu England ikiwa imebakiza mechi mbili kumalizika, kikosi hicho cha Jose Mourinho kinatakiwa kushinda zote mbili ili kupata pointi zote zitakazowaweka kwenye nafasi nzuri.

Na Kane amewaambia wachezaji wenzake kwamba, wanatakiwa kupigana haswa ili kuhakikisha wanashinda mechi mbili zilizobaki dhidi ya Leicester na Crystal Palace, lakini vinginevyo watakuwa wamekosa nafasi ya kucheza mashindano ya Ulaya msimu ujao.

"Kuifunga Newcastle ulikuwa ushindi mzuri kwetu," alisema akiiambia tovuti ya Spurs.

"Tulisema mwanzo, mechi tatu ni za ushindi wa lazima, tunatakiwa tushinde mechi tatu kama tunataka kufuzu kucheza Ligi ya Europa."

HABARI MICHEZO

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# MESSI: MADRID ILISTAHILI KOMBE

●●●Mshambuliaji huyo aeleza Barca ilijitoa yenyewe kwenye mbio za kuwania taji hilo baada ya ...

**BARCELONA, Hispania**

MSHAMBULIAJI Lionel Messi amesema Real Madrid walistahili kuwa mabingwa wa LaLiga msimu huu, baada ya timu yake ya Barcelona kujiondoa yenyewe kwenye mbio za kuwania taji hilo.

Barca waliwarahisishia ubingwa huo Real Madrid wakati walipokubali kichapo cha mabao 2-1, na kuwafanya wapinzani wao kulitwaa taji hilo juzi Alhamisi ikiwa ni mara ya kwanza kwa kipindi cha misimu mitatu.

Nahodha huyo wa Barca, Messi, ambaye alifunga bao la kusawazisha kwa kikosi hicho cha kocha, Jose Arnaiz kabla ya Roberto Torres kufunga goli la ushindi kwa Osasuna, na kuwafanya miamba hao wa Katalunya kuachia taji kwa wapinzani wao Real Madrid, ambao waliibuka na ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Villarreal.

Na baada ya mchezo huo Messi aliiambia Movistar: "Tumekuwa tukilikimbiza taji kwa msimu mzima, lakini hatukuwa na kiwango bora.

"Leo (juzi) haikuwa kazi rahisi kutafuta nafasi ya kumfunga golikipa. Sikujua kama mchezo wetu ungekuwa mgumu kwa kiasi hiki na tulijaribu kutulia na kujaribu kusukuma mashambulizi mbele bila mafanikio.

"Nafikiri Real Madrid walifanya kile walichokifanya. Wamefanya vizuri tangu kurudi kwa ligi baada ya kusimama.

"Bila shaka tuna majeruhi mengi na tumepoteza pointi nyingi kwenye michezo ambayo hatukutakiwa kufanya hivyo na sasa tutatakiwa kujitafakari sisi wenyewe.

"Tupo kwenye kipindi cha majira ya joto, tunatakiwa kuangalia makosa yetu ya nyuma ili tuweze kuwa na msimu mpya.

"Ukiangalia nyuma, sisi tulikuwa na wakati mzuri zaidi wa kulitwaa taji msimu huu, lakini sasa Madrid walistahili.

"Tunatakiwa kuangalia nyuma namna gani tulivyocheza na kipi tulichokifanya na kwa uhakika kabisa sisi wenyewe tunapaswa kujilaumu.

"Ni vigumu kucheza kwa namna tulivyocheza ili tuweze kushinda, kwa hakika kabisa, hatukuwa kwenye nafasi nzuri. Tujitafakari na tuangalie namna gani msimu ujao mambo yakatavyokuwa."

## KWA UFUPI

**HAVERTZ AEKEWA NGUMU**
BAYER Leverkusen imeshakubali kiungo wake, Kai Havertz (21), ameamua kwenda kujiunga na Chelsea lakini klabu hiyo ya Bundesliga inataka Mjerumani huyo aondoke mwishoni mwa Agosti. ***(Star)***

**TAGLIAFICO ANUKIA CITY**
BEKI wa kushoto wa Ajax na Timu ya Taifa ya Argentina, Nicolas Tagliafico (27), anatajwa ndio chaguo la kwanza la Manchester City katika dirisha la usajili la majira ya joto. ***(Sports Illustrated)***

**THIAGO AIKACHA BAYERN**
KIUNGO Mhispania, Thiago Alcantara (29), anaamini atakamilisha mkataba wa kujiunga na Liverpool baada ya kukataa kusaini mkataba mpya na klabu yake ya Bayern Munich. (Mirror)

**SARR AKARIBIA ARSENAL**
ARSENAL inajiandaa kumsajili beki wa Timu ya Taifa ya Vijana ya Ufaransa ya umri chini ya miaka 21 (U-21), Malang Sarr lakini nyota huyo wa Nice ambaye atakuwa huru katika dirisha la usajili anawaniwa na klabu mbalimbali za Italia na Ujerumani. ***(Sun)***

**CARRERAS, UNITED SAFI**
MANCHESTER United imefikia makubaliano ya kumsajili beki wa kushoto wa Real Madrid, Alvaro Fernandez Carreras (17), ambaye anatarajiwa kusaini mkataba wa miaka mitano na klabu hiyo ya Old Trafford. ***(AS - in Spanish)***

**POCHETTINO AGOMBEWA ITALIA**
KOCHA wa zamani wa Southampton na Tottenham, Mauricio Pochettino ametajwa katika orodha ya makocha wanaowaniwa na Inter Milan pamoja na Juventus wakati klabu hizo za Italia zikijiandaa kuwafukuza Antonio Conte na Maurizio Sarri ifikapo mwishoni mwa msimu. ***(Telegraph)***

**CONTE AMTAKA KANTE**
KOCHA wa Inter Milan, Antonio Conte atalazimika kuishawishi bodi ya klabu hiyo kukubaliana na mshahara anaotaka kulipwa N'Golo Kante (29), ili wafanikishe usajili wa kiungo huyo Mfaransa anayekipiga kwenye kikosi cha Chelsea. ***(SempreInter)***

**BELLINGHAM AFAULU**
KIUNGO Jude Bellingham (17), amekamilisha vipimo vya afya katika klabu ya Borussia Dortmund kabla ya mchakato wake wa uhamisho kukamilika lakini ataendelea kuitumikia Birmingham mpaka mwisho wa msimu. ***(Sky Sports)***

**SPURS KUMKOSA AURIER**
TOTTENHAM itamaliza msimu bila ya beki wa Timu ya Taifa ya Ivory Coast, Serge Aurier (27), baada ya kurejea Ufaransa kuhudhuria msiba wa kaka yake. ***(Evening Standard)***

**EVERTON YAMTAKA ALLAN**
EVERTON imewasilisha ofa ya kumsajili beki wa Napoli, Allan, lakini klabu hiyo ya Italia inaonyesha haitaki kumtoa mchezaji huyo kutoka Brazil mwenye umri wa miaka 29. ***(Sport Witness)***

**PALACE MAMBO SAFI**
KOCHA Roy Hodgson amesema ujio wa wachezaji wapya katika kikosi cha Crystal Palace kutaifanya klabu hiyo maarufu The Eagles kuwa na mafanikio kwenye msimu ujao na kuwafanya kumaliza kwenye nafasi 10 za juu. ***(Evening Standard)***

**TORRES KUTUA CITY**
MABOSI wa Manchester City wamefikia makubaliano binafsi na winga wa Valencia Mhispania, Ferran Torres, ambaye ana umri wa miaka 20. ***(Eurosport)***

HABARI MICHEZO

# GWAMBINA, DODOMA FAINALI YA KIBABE FDL

**Na Saada Akida**

TIMU ya Gwambina FC inatarajia kukutana na Dodoma Jiji katika mechi ya fainali ya Ligi Daraja la Kwanza itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Azam Complex uliopo, Chamazi jijini, Dar es Salaam.

Gwambina FC kutoka jijini Mwanza na Dodoma Jiji ya makao makuu, tayari zimeshapanda daraja na msimu ujao zitacheza Ligi Kuu Tanzania Bara baada ya kuongoza katika Kundi A na B.

Mechi hiyo ya fainali inatarajiwa kuwa na ushindani kutokana na rekodi ambazo timu hizo zimeweka katika michezo yake ya hatua ya makundi.

Kocha Mkuu wa Dodoma Jiji FC, Mbwana Makata, alisema kikosi chake kimefanya maandalizi mazuri kuelekea mchezo huo na anahitaji kuona wanajenga heshima kwa kupata ushindi.

Makata alisema mechi zote walizocheza ni ngumu na wako tayari kukutana na changamoto yoyote katika mchezo huo.

"Ninawaheshimu wapinzani wetu, utakuwa mchezo mgumu na wa aina yake, tunatarajia kukutana na ushindani mkubwa, kwa sababu kila timu ina wachezaji wazuri na ambao wamepata uzoefu wa kupambana," alisema Makata.

Nahodha wa timu hiyo, Mbwana Hamis, aliliambia gazeti hili wachezaji wote wana molari ya kutaka 'kulinda heshima' na kuweka historia ya kutwaa kombe hilo pamoja na kuvaa medali.

"Tunahitaji kuwaonyesha tumepambana kufika hapa, tumejiandaa vizuri kwa ajili ya mechi ya fainali hiyo," alisema nahodha huyo.

Novatus Fulgence, Kocha Mkuu wa Gwambina, alisema kikosi chake kimejipanga imara na kinaamini kitamaliza msimu kwa mafanikio na kuchukua taji hilo ni moja ya mikakati yao.

Alisema katika mchezo huo wa fainali atawakosa wachezaji wawili, Salum Kipanga na Pastory Athanas ambao ni majeruhi.

Kocha huyo alisema anawaheshimu wapinzani wake, lakini atautumia mchezo huo kama sehemu ya maandalizi ya msimu wake mpya wa Ligi Kuu Tanzania Bara.




Mkurugenzi wa Utawala na Udhibiti SportPesa, Tarimba Abbas (kushoto), akimkabidhi mfano wa hundi ya Sh. milioni 288.9 mshindi wa Jackpot ya SportPesa, Jamal Abdallah ambaye ni shabiki wa Yanga. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Shabiki Yanga ashinda SportPesa

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Michezo na Burudani ya SportPesa Tanzania jana, ilimkabidhi mshindi wa Jackpot SportPesa, Jamal Abdallah (26), zawadi ya Sh. milioni 288.9 baada ya kubashiri kwa usahihi mechi 13.

Hii ni awamu ya nne kwa Jackpot ya SportPesa kupata mshindi kutoka Wilaya ya Ilala jijini, Dar es Salaam baada ya washindi wengine watatu kujizolea mamilioni kupitia ubashiri huo wa michezo.

Akizungumza jijini jana, wakati wa kumtangaza mshindi huyo, Mkurugenzi wa Utawala na Udhibiti SportPesa Tanzania, Tarimba Abbas alisema Jamal ameshinda Jackpot hiyo baada ya kubashiri mechi 13 zilizochezwa mwishoni mwa wiki kwa usahihi.

"Mpaka sasa SportPesa imeshatoa zaidi ya Sh. bilioni 1.8 kwa washindi wanne wa Jackpot kwa kubashiri kwa usahihi mechi 13. Pia tangu tuanze biashara Mei, 2017 hadi leo hii washindi wa Jackpot na bonasi wamelipwa zaidi ya Sh. bilioni 8.2.

Tarimba alisema wanafurahi kuona katika kipindi cha miaka mitatu mfululizo wanabadili maisha ya Watanzania mbalimbali na kuongeza familia ya mamilionea.

"SportPesa ni kampuni inayofuata taratibu zote ili kuhakikisha sheria zilizowekwa na bodi ya michezo ya kubahatisha zinafutwa ikiwa pamoja na kulipa kodi. Kodi iliyolipwa kwa washindi wote wa Jackpot waliopatikana kuanzia 2017 tu wameweza kurudisha kodi kwa serikali kwa zaidi ya shilingi bilioni 1.6.

"Nitoe rai kwa Watanzania wote na wapenda michezo kuwa SportPesa ipo kwa ajili ya kuwaburudisha hasa kwenye ubashiri wa mipira ya miguu na mara zote mshindi uwekewa pesa zake kwenye akaunti yake papo hapo," alisema Tarimba.

Jamal alisema, "Sikutegemea kama nitashinda maana niliwekea mikeka zaidi ya kumi, hivyo nilitegemea kupata bonasi na sio Jackpot.

"Hizi pesa nilizoziweka kwa hivi sasa sitazitumia na badala yake nitaziweka kwanza benki kwa muda huku nikifikiria nini cha kufanya, kwa sababu hizi pesa ni nyingi kwani utulivu mkubwa unahitajika.

"Mimi ninajishughulisha na ujasiriamali kwa hivi sasa, hivyo kupitia ushindi wangu huu ninaamini nitafanikisha mahitaji yangu muhimu."

"Nashabikia sana timu ya Yanga na nimefurahi sana SportPesa kuniletea wachezaji kama 'suprise' ya leo."

## Mbao yaingia kwenye rekodi Bara

**Na Adam Fungamwango**

USHINDI wa mabao 3-2 ilioupata Mbao FC katika mechi ya Ligi Kuu Bara dhidi ya Simba kwenye Uwanja wa Taifa jijini, Dar es Salaam juzi, umeifanya timu hiyo kushinda mechi tano mfululizo, huku straika wake hatari, Waziri Junior akifunga mechi nne mfululizo.

Mbao, ambayo iko kwenye kampeni kabambe ya kuhakikisha inasalia Ligi Kuu Tanzania Bara, lakini pamoja na ushindi wa tano mfululizo bado iko pale pale kwenye nafasi ya 19, ikiwa imefikisha pointi 38, lakini Kocha Mkuu wa timu hiyo, Fred Minziro ametamba hawatashuka daraja.

Minziro alisema kama 'hesabu' zao zitakwenda vema, timu yake itaendelea kushiriki ligi hiyo na watapambana hadi dakika ya mwisho ya msimu huu.

"Simba ni timu nzuri, hilo halipingiki, lakini niliwaambia vijana wangu wapambane, kwa sababu wapinzani wetu hawana cha kupoteza, sisi ndiyo tunataka ushindi kwa lazima ili tukae sehemu salama," alisema Minziro.

Naye mfungaji wa bao la pili, Waziri alisema nia yao ni kupata pointi nyingine tisa ili kufikisha pointi 47 ambazo wana uhakika timu nyingi ambazo pia zinapambana kutoshuka daraja, hawatafikisha.

"Kufunga kwangu magoli kunatokana na ushirikiano wangu na wachezaji wenzangu, lakini mimi mwenyewe nina mazoezi yangu binafsi, hivyo najiwekea malengo," alisema waziri ambayo tayari amefikisha magoli 11 msimu huu.

## Simba Queens, Yanga dimbani

**Na Saada Akida**

LIGI Kuu ya Wanawake Tanzania inatarajiwa kuendelea katika viwanja sita nchini ambapo vinara Simba Queens watakuwa ugenini kuwakabili Kigoma Sisterz kwenye Uwanja wa Lake Tanganyika mkoani Kigoma huku Yanga Princess ikiwakaribisha Ruvuma Queens.

Simba Queens wanaongoza ligi hiyo wakiwa na pointi 41, huku mabingwa watetezi JKT Queens wenye pointi 36 wakifuatia wakati Panama Queens inaburuza mkia ikiwa na pointi nne.

Vinara Simba Queens watashuka dimbani leo wakiwa na kumbukumbu nzuri ya kuwafunga watani wao wa jadi, Yanga Princess mabao 5-1 halafu ikawapa Marsh Queens kichapo cha mabao 5-0, katika mchezo uliochezwa kwenye Uwanja wa Nyamagana jijini, Mwanza.

Kocha Mkuu wa Simba Queens, Mussa Hassan `Mgosi` alisema wanahitaji pointi tatu muhimu katika kile mechi ili kufikia malengo yao ya msimu ubingwa wa msimu huu.

Mgosi alisema maandalizi yao yamekwenda vizuri na hakuna mchezaji ambaye ni majeruhi katika kikosi chake. Michezo mingine ya ligi hiyo itakayochezwa leo ni kati ya Tanzanite SC dhidi ya TSC Queens, Baobab Queens vs Allinace Girls, JKT Queens vs Panama Queens na Marsh Queens wataikaribisha Mlandizi Queens.

Michezo
Jumamosi Julai 18, 2020
Nipashe



## Messi: Madrid ilistahili kombe

HABARI UK 22



Beki wa Simba, Erasto Nyoni (kulia), akiwania mpira dhidi ya mshambuliaji wa Mbao FC, Ndaki Robert katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa Taifa jijini, Dar es Salaam juzi usiku. Mbao ilishinda mabao 3-2. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# YANGA DIMBANI KUSAKA HESHIMA

## ●●●Kocha wake aeleza kuikosa nafasi ya pili itakuwa ni 'pigo' jipya wakati wakiivaa Mwadui...

**Na Faustine Feliciane**

WAKATI bado machungu ya kufungwa na watani zao na kutolewa kwenye mashindano ya Kombe la FA hayajaisha, Kocha Mkuu wa Yanga, Luc Eymael amesema litakuwa 'pigo' lingine endapo timu yake itashindwa kumaliza katika nafasi ya pili kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu.

Baada ya mapema kujiondoa kwenye mbio za ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara na taji hilo kwenda kwa watani zao, Simba, ndoto za Yanga kushiriki michuano ya kimataifa zilipotea wiki iliyopita ilipokubali kichapo cha magoli 4-1 kutoka kwa Wekundu wa Msimbazi.

Eymael alisema kwa sasa hakuna taji ambalo wanaliwania, lakini wamejipanga kupambana ili kumaliza kwenye nafasi hiyo ambayo pia inawaniwa na Azam FC pamoja na Namungo ya Lindi.

Mbelgiji huyo alisema ukiondoa mipango ya kuhakikisha wanashinda mechi zao tatu zilizobaki, lakini tayari mikakati ya kusuka kikosi chao cha msimu ujao imeshaanza.

"Sitaki kuzungumza kwa kirefu sana, lakini kwa sasa tunataka kuona tunamaliza nafasi ya pili, ila tumeshaanza mipango kwa ajili ya msimu ujao, msimu huu umekuwa na maumivu kwa mashabiki wetu, tunawaahidi msimu ujao utakuwa wa tofauti zaidi kwetu," alisema Eymael.

Kocha huyo aliongeza anaupa umuhimu mkubwa mchezo wao wa leo dhidi ya Mwadui FC kwa sababu matokeo ya ushindi yatawasaidia kufikia malengo yao.

"Tunauangalia mchezo ujao kwa nafasi kubwa, matokeo ya ushindi pekee ndiyo tunayoyahitaji, tunafikiria pointi tatu kutoka katika mchezo huo. Baada ya msimu huu kumalizika na kufanya tathmini, kurekebisha mapungufu yaliyopo ya kila idara, tutaingia tukiwa imara na tofauti," Eymael alisema.

Hata hivyo, Eymael jana alikataa kuzungumza chochote kuhusiana na sintofahamu ya kiungo mshambuliaji wa timu hiyo Bernard Morison.

Meneja wa timu hiyo, Abeid Mziba, alisema wachezaji wote wapo kwenye hali nzuri kuelekea mchezo huo dhidi ya Mwadui FC.

Mziba alisema Yanga inajipanga na inaipa umuhimu michezo iliyobaki licha ya kupoteza nafasi ya kushiriki mashindano ya kimataifa msimu ujao.

"Kuhusu Morrison siwezi kusema chochote, naomba tuzungumzie timu na si mchezaji mmoja mmoja," alisema meneja huyo.

Taarifa zilizopatikana jijini zinasema nyota huyo wa kimataifa kutoka Ghana hajahudhuria mazoezi na hajaungana na wenzake tangu baada ya kufanyiwa mabadiliko katika mchezo wao uliopita dhidi ya Simba.

Mechi nyingine za Ligi Kuu Tanzania Bara zitakazochezwa leo ni kati ya Mtibwa Sugar dhidi ya KMC, wakati Namungo watakaikaribisha Prisons huku Ndanda wakiwaalika Mbeya City na Biashara United watavaana na Coastal Union kwenye Uwanja wa Karume mjini Musoma.

Kagera Sugar watawakaribisha Polisi Tanzania kwenye Uwanja wa Kaitaba, Bukoba, huku kesho mabingwa Simba wakivaana na Alliance FC kutoka jijini, Mwanza.

# SIMBA 'ORIGINAL' KUIVAA ALLIANCE

**Na Somoe Ng'itu**

BAADA ya kupoteza mchezo uliopita dhidi ya Mbao FC, mabingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba wanatarajia kuteremsha kikosi 'imara' katika mechi ya ligi hiyo dhidi ya Alliance FC kutoka jijini Mwanza itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa Taifa.

Simba iliwapa mapumziko ya siku mbili, nyota wake walioanza katika mechi ya hatua ya nusu fainali dhidi ya watani zao, Yanga ambayo ilimalizika kwa Wekundu wa Msimbazi kushinda mabao 4-1.

Meneja wa Simba, Patrick Rweyemamu, alisema maandalizi ya mechi ya kesho yanaendelea vema na wachezaji wote waliokuwa wamepewa mapumziko, wamerejea kikosini.

Rweyemamu alisema wanatarajia mechi hiyo pia itakuwa na ushindani kwa sababu Alliance inahitaji kujiweka kwenye nafasi salama kwa sababu bado timu zitakazoshuka daraja hazijafahamika.

**"Timu ambazo ziko salama hazizidi tano, dakika za lala salama lolote linaweza kutokea, yaliyotokea mechi iliyopita yamepita, mchezo wa Jumapili utakuwa na mipango tofauti," alisema meneja huyo.**

Mechi hiyo ya kesho itakuwa ya mwisho kwa mabingwa hao jijini na baada ya hapo itasafiri kuwafuata Coastal Union na itafunga pazia la msimu kwenye Uwanja wa Chuo cha Ushirika, Moshi dhidi ya wenyeji, Polisi Tanzania ifikapo Julai 26, mwaka huu.

9 770856 541002 >

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042